# BARAZA KUU LA WAISILAM WA TANZANIA (BAKWATA)





## OFISI YA MUFTI

# STADI ZA MAISHA KWA MWANAMKE WA KIISLAM

**KOZI : STADI ZA MAISHA KWA MWANAMKE WA KIISLAM**

**KWA NJIA YA MASAFA**

**www.bakwataonlineacademy.ac.tz**

**MADA KUU**

- NAFASI YA MWANAMKE KATIKA UISLAM
- WAJIBU WA MWANAMKE NDANI YA FAMILIA
- MWANAMKE KAMA MWALIMU KIMALEZI
- CHAKULA NA LISHE NA UMUHIMU WAKE KIAFYA
- UJASIRIAMALI NA UCHUMI KWA MWANAMKE

**BAKWATA MPYA: JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA**



# Contents


UTANGULIZI ....................................................................................................................6

MWANAMKE WA KIISLAM NA ELIMU ...................................................................6

MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA ELIMU ......................................................................6

Katika Uislamu Hakuna Elimu ya Dini na Dunia ...........................................6

Elimu yenye Manufaa .........................................................................................9

UISLAM UMEMPA HESHIMA MWANAMKE ..................................................................10

Mwanamke Mshirika Katika Maisha ...........................................................11

MAISHA YA FAMILIA YA MKE NA MUME ......................................................14

MTAZAMO WA KIJAMII JUU YA MWANAMKE WA KIISLAM..............................16

KAZI NA BIASHARA KWA MWANAMKE WA KIISLAM..........................................17

Bi Khadija bint Khuwailid(R.A) Alikuwa Mfanya Biashara ..............................17

WAJIBU WA MWANAMKE NDANI YA FAMILIA ..................................................19

MAJUKUMU YA MWANAMKE KIMAISHA ............................................................20

CHAKULA NA LISHE ......................................................................................21

Faida za chakula kwa binadamu: ..............................................................21

Virutubishi, umuhimu na vyanzo vyake ...........................................................22

Kabohaidreti ....................................................................................................22

Protini ..............................................................................................................22

Mafuta ..............................................................................................................23

Vitamini.............................................................................................................23

Madini...............................................................................................................24

Vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi: ...............................................................24

• Vyakula vya mikunde na vyenye asili ya wanyama: .........................................25

• Mafuta na sukari:.............................................................................................25

VITAFUNWA VYEPESI .............................................................................27

POP CORN NA KARANGA.............................................................................27

VITAFUNWA ASILIA ........................................................................................27

MIHOGO YA KUCHEMSHA NA SAMAKI WA KUKAANGA ........................................27

JINSI YA KUPIKA CHAPATI LAINI ......................................................................28

Maandazi ya Mayai na Maziwa.............................................................................29

Mkate wa maboga, nazi, na maziwa ......................................................................30

Kebab za nyama...................................................................................................32

Karanga za mayai ................................................................................................33

Sambusa za nyama ...............................................................................................34

Kashata za nazi ....................................................................................................35

UJASIRIAMALI NA UCHUMI................................................................................35

Dhana ya uchumi katika uisilam..........................................................................36

BIASHA NA HALI HALISI YA KIBIASHARA...........................................................37

BIASHARA NA MATUMIZI SAHIHI YA MUDA .........................................................38

Maana ya kutunza muda (Time management) ...... 38
UJASIRIAMALI NI NINI? ...... 38
MWANZO WA UJASIRIAMALI: ...... 39
SIFA ZA MRADI WA KIJASIRIAMALI. ...... 39
MJASIRIAMALI MZURI (mambo ya kuzingatia) ...... 39
MISINGI YA UJASIRIAMALI. ...... 39
MAONO (VISION) ...... 40
(MISSION) ...... 40
Sababu ya kufanya mradi huo na si mingine (statement of purpose) lazima ionyeshe kutatua tatizo au kutumia fursa iliyopo. ...... 40
MALENGO ...... 40
Ni mambo unayotaka kuyafikia au kuyapata pia unaweza kuweka na wakati. ...... 40
MFUMO WA MALENGO. ...... 40
FAIDA ZA UJASIRIAMALI ...... 40
MJASIRIAMAJI ANAJENGWAJE ...... 40
FULSA ...... 40
JE UNAWEZA KUWA MJASIRIAMALI ...... 40
AINA ZA UZALISHAJI MALI/BIASHARA ...... 41
BIASHARA ZA MTAJI MDOGO ZENYE FAIDA KUBWA ...... 41
1. KUNUNUA NA KUUZA BIDHAA ...... 42
2. KUPIKA KWA ODA ...... 42
3. KUUZA JUISI NA ICE CREAM ...... 42
4. KILIMO CHA MBOGAMBOGA ...... 42
5. UFUGAJI WA NDEGE (KUKU, BATA, N.K) ...... 42
6. UREMBO (MAKEUP, KUSUKA & KUCHA) ...... 43
7. KUPANGA SHEREHE/MATUKIO (EVENT PLANNING) ...... 43
8. USHONAJI NGUO ...... 43
9. KUFUNDISHA ...... 43
10. KUTENGENEZA SIMU/KOMPYUTA ...... 43
11. UNYOZI WA NYWELE kwa WANAWAKE NA WATOTO TU ...... 43
12. KUUZA VOCHA ZA SIMU ...... 44
13. UFUGAJI WA SAMAKI ...... 44
14. KUKUZA MITI YA MAUA ...... 44
15. KUFANYA USAFI MAJUMBANI NA MAOFISINI ...... 44
16. KOCHA WA MAZOEZI KWA WANAWAKE WENZAKO ...... 44
17. KUPAMBA MAHARUSI ...... 44
18. KUWAUZIA WATU BIDHAA ZAO ...... 44
19. KUTENGENEZA SABUNI ZA MAJI ...... 44
JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA KUNAWIA MIKONO ...... 45
HATUA ZA KUTENGENEZA ...... 45

KUTENGENEZA SABUNI YA CHOONI ........ 45
JINSI YA KUTENGENEZA/ HATUA ZA KUTENGENEZA ........ 45
UTENGENEZAJI SABUNI ZA MCHE ........ 46
JINSI YA UTENGENEZAJI SABUNI ZA GWANJI/MCHE MALIGHAFI ........ 46
MFANO WA BOX LA KUTENGENEZEA SABUNI YA MCHE ........ 47
BIASHARA YA VIUNGO KWA AJILI YA VINYWAJI NA CHAKULA ........ 48
SPICES NI TIBA ........ 52
VIFUNGASHA NA KUWEKA LEBEL ........ 52
FAIDA YA KUFUNGASHA NA KUWEKA LEBO NZURI KWENYE SPICES ........ 53
UTUNZAJI WA SPICES ZILIZOTAYARI ........ 53
UTAFUTAJI WA MASOKO ........ 53
Soko ni nini? ........ 53
KUTUMIA SIMU NA MITANDAO YA KIJAMII KUTANGAZA BIASHARA ........ 56
LIPI LA KUFANYA KUTANGAZA BIASHARA MTANDAONI? ........ 57
BLOG NA TOVUTI(website) KATIKA KUTANGAZA BIASHARA ........ 58
MTIHANI WA KWANZA 2021- MTIHANI WA WAZI ........ 60

# UTANGULIZI

Kutokana na dunia ya sasa mambo mengi kuhitaji maarifa, inatubidi tujifunze kila mara ili tuweze kuendelea kumcha Mwenyezi Mungu wa pekee, aliyetakasika na wakati huo huo tukimudu maisha yenye mabadiliko.

## MWANAMKE WA KIISLAM NA ELIMU

Katika Uislam, elimu ni muhimu sana. Aya ya kwanza ndani ya Qur'ani iliagiza kusoma " Iqra'a"( "Soma!") "Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba." (96:1) Na amri hii haikutofautisha kati ya wanaume na wanawake. Mke wa kwanza wa Mtume Muhammad(Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) Bi Khadeeja , alikuwa mwanamke mwenye ujuzi mbali mbali ikiwemo biashara(business), Mtume Muhammad aliwasifu wanawake wa Madina kwa ajili ya kutafuta kwao elimu: "Wanawake wa *Ansari walijitahidi kujifunza dini na satdi za maisha mbali mbali* , Mtume Muhammad aliwaambia waislam hivi:

- "Kutafuta elimu/ ujuzi ni wajibu kwa Waislamu wote, wanaume na wanawake."
- "Tafuta ujuzi, tangu utotoni hadi kaburini." (Elimu haina mwisho katika uislam)
- "Tafuta elimu hata ikiwa ni China."( Hii inaonyesha popote ujuzi muhimu utafutwe)
- "Mtu anayetoka katika kutafuta elimu/ujuzi yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu, mpaka atakaporejea."

Mifano hiyo juu ni kuonyesha umuhimu wa kusoma na kupata maarifa kwa waislam bila kubagua wanawake na wanaume.

Hakika, katika historia, wanawake wengi wa Kiislam walihusika katika kuanzishwa kwa taasisi za elimu.

Mfano ni Fatima al-Fihri, ambaye alianzisha Chuo Kikuu cha Al-Karaouine mnamo 859 CE. Chuo kikuu hiki kinabaki, kwa mujibu wa UNESCO kama kumbu kumbu, chuo kikuu cha zamani zaidi duniani.

# MTAZAMO WA UISLAMU JUU YA ELIMU

## Katika Uislamu Hakuna Elimu ya Dini na Dunia

Kwa mtazamo wa Uislamu (Qur-an na Sunnah) hapana mgawanyo huu wa elimu kwa sababu za msingi zifuatazo:

**Kwanza**, Nabii Adam (a.s) katika kuandaliwa yeye na kikazi chake kuwa Makhalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni alifundishwa majina ya vitu vyote kama Qur-an inavyoainisha:
"Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha Adam majina ya vitu vyote…" (2:31). Majina ya vitu vyote hapa kama tulivyotangulia kusema inaashiria fani zote za elimu zitakazomuwezesha binaadamu kuendea kila kipengele cha maisha yake na kufikia malengo tarajiwa. Pamoja na kufundishwa majina ya vitu vyote, pia Adam (a.s) na kizazi chake waliahidiwa na Mola wao kuletewa mwongozo utakaowawezesha kutumia fani mbali mbali za taaluma walizonazo

kwa kufuata utaratibu utakaowapelekea kukiendea kila kipengele cha maisha yao kwa furaha na amani: "Tukasema: Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uwongozi wangu huo, haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika." (2:38).

Lakini wale watakaotumia taaluma mbali mbali walizonazo katika kuendea kila kipengele cha maisha yao ya kila siku ya kibinafsi na kijamii bila ya kufuata mwongozo wa Allah (s.w) kupitia kwa Mitume wake na Vitabu vyake, wataishi maisha ya huzuni na khofu na katika maisha ya akhera watakuwa na adhabu kali: "Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa motoni, humo watakaa milele." (2:39)

Kwa mujibu wa maelezo haya tunajifunza kuwa fani zote za elimu (majina ya vitu vyote) ambazo amezifundisha Allah (s.w) pamoja na mwongozo maalumu kutoka kwake, vinahitajika kwa binaadamu ili kumuwezesha kuishi maisha ya furaha na amani hapa duniani na huko akhera. Hivyo hapana mwenye uwezo wa kutenganisha maisha ya dini na dunia au elimu ya dini na dunia.

**Pili,** Amri ya kusoma (kutafuta elimu) aliyopewa Mtume (s.a.w) na umma wake, haibagui elimu ya dini na dunia.
Vinginevyo fani yoyote ya elimu inayomuwezesha binaadamu kusimamisha ukhalifa wa Allah (s.w) katika jamii na kufikia lengo la kuumbwa la kumuabudu Allah (s.w) inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake inapaswa isomwe kwa juhudi zote.

**Tatu,** chanzo cha fani zote za elimu ni Allah (s.w) kama Qur-an inavyosisitiza:
"Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha (Binaadamu fani zote za elimu) kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu (chungu ya mambo) aliyokuwa hayajui". (96:3-5) Kwa mujibu wa aya hizi hapana fani yoyote ya taaluma iliyoasisiwa na binaadamu. Zote fani zinatoka kwa Allah mmoja aliyetakasika

**Nne,** katika Qur-an tunafahamishwa kuwa wanaomcha Allah (s.w) ipasavyo na kumuogopa ni wale wataalamu (ulamaa) waliozama katika fani mbali mbali za elimu. Kwa mujibu wa Qur'an fani hizi mbali mbali haziishii tu kwenye zile fani zinazotazamwa kwa mrengo wa kidini kama vile fiqh, Tawhiid, n.k. bali fani zote za elimu zinazo muwezesha binaadamu kutafakari kwa undani juu ya kuwepo Allah (s.w) na daraja ya utukufu wake, hasa zile fani za kisayansi zinazohusiana na maumbile. Hebu turejee aya zifuatazo:

“Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji toka mawinguni! Na kwayo tumeyatoa matunda yenye rangi mbali mbali. Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbali mbali, na (mengine) myeusi sana.” (35:27)

“Na katika watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni mbali mbali. **Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanavyuoni).** Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Msamehevu.” (35:28)

Katika aya hizi tunajifunza kuwa wenye kumcha Allah (s.w) ipasavyo na katika kiwango cha juu cha unyenyekevu ni wale waumini waliobobea katika taaluma mbali mbali (maulamaa). Je, maulamaa waliotajwa katika aya hizi ni wale tu waliobobea kwenye taaluma zinazoitwa za kidini kama vile fiq-h, Qur-an na Hadith?
Maulamaa waliopigiwa mfano katika aya hizi ni wale waliozama katika fani ya Hali ya Hewa (Meteorologist), Maulama waliozama katika uchunguzi wa wanyama (Zoologist), maulamaa waliozama katika fani ya matunda (Horticulturist), Maulamaa waliozama katika

fani ya Madini (Geologists) na Maulamaa waliozama katika fani ya kuchunguza watu walivyo kimaumbile, rangi, n.k. (Anthropolagist).
Pia katika aya nyingi za Qur-an binaadamu amesisitizwa kuyafanyia utafiti mazingira ya mbingu na ardhi ili kumtambua Mola wake na kumuabudu ipasavyo.

**Tano,** katika Qur-an Allah (s.w) anatufahamisha kuwa waumini waliobobea kwenye elimu wana daraja kubwa zaidi kuliko waumini wengine: "… Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa elimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote." (58:11)

Aya hii haijabagua wenye elimu. Hivyo yeyote yule mwenye taaluma inayomuwezesha kumcha Mola wake na kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha yake na ikamuwezesha kuchangia katika kusimamia Uislamu katika jamii atakuwa na daraja zaidi kuliko wale wasio na taaluma hiyo kama Qur-an inavyozidi kusisitiza:

**"… Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi." (49:13)**

Aya hiyo inajumuisha wanawake na wanaume, muhimu ni kumcha Mwenyezi Mungu mmoja wa pekee aliyetakasika.

**Sita**, hatuoni mgawanyo wa elimu katika Hadith mbali mbali za Mtume (s.a.w) zinazozungumzia elimu. Kwa mfano Mtume (s.a.w) aliposema: "Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila Muislamu mwanamume na kila Muislamu mwanamke." (Ibn Majah), hakubagua elimu. Pia rejea Hadith zifuatazo: Anas (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Mwenye kutoka nje kutafuta elimu yuko katika njia ya Allah mpaka atakapo rejea. (Tirmidh).

Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema:Yeyote atakayeulizwa juu ya jambo alilojifunza kisha akaficha (akakataa kutoa elimu ile) atavalishwa mshipi (mkanda) wa Moto siku ya Kiyama." (Ahmad, Abu Daud, Tirmidh na Ibn Majah). Pia tunajifunza katika historia kuwa Mtume (s.a.w) aliwaacha huru mateka wa vita vya Badr kwa yule aliyeweza kujikomboa kwa kuwafunza kusoma na kuandika watoto kumi wa Waislamu. Hadith hizi zinadhihirisha kuwa Mtume (s.a.w) naye hakuigawanya elimu katika elimu ya dini na elimu ya dunia. Bali Mtume (s.a.w) amewahimiza Waislamu kutafuta elimu yenye manufaa kwa jamii popote pale inapopatikana. "Tafuteni elimu hata China" (Baihaqi).

Laiti kama pangelikuwepo na mgawanyo wa elimu na kuwa elimu ya lazima kutafutwa na Waislamu ni ile iitwayo "elimu ya dini" kwanini Mtume (s.a.w) aliwaamuru waende China wakati wahayi ulikuwa unamfuata yeye alipo? Ilikuwa inatosha wao kubaki na Mtume Makkah au Madina na asiwatume tena kwenda China kutafuta elimu. Hivyo, kutokana na hoja hizi sita, Uislamu hautambui mgawanyo wa elimu kwenye tapo la elimu ya dini na elimu ya dunia.

Elimu ya Maarifa ya Uislamu, itakayompelekea mja kumtambua Mola wake vilivyo na kumuabudu inavyostahiki katika kila kipengele cha maisha ni faradh muhimu. Kwa maana nyingine ni faradh kwa kila Muislamu kuujua Uislamu vilivyo na kujitahidi kuutekeleza kwa kadiri ya uwezo wake katika kila kipengele cha maisha. Elimu juu ya fani mbalimbali zinazohitajika katika maisha ya jamii ni faradhi ya jumla kwa jamii ya Kiislamu.

Kwa mfano ni faradhi kwa jamii ya Kiislamu kuwa na madaktari, wahandisi, wanasheria,

wanasiasa, wanauchumi, waalimu na wataalamu wengineo katika kila fani ya maisha ya jamii wa kutosha kukidhi mahitajio ya jamii katika kuendea nyanja zote za maisha.

Ikitokezea Waislamu wamezembea kiasi cha kushindwa kutoa wataalamu wanaohitajika kuendesha kila fani ya maisha ya jamii mpaka inapelekea Waislamu kushindwa kumuabudu Mola wao ipasavyo katika kila kipengele cha maisha, jamii yote ya Waislamu itakuwa katika lawama (itapata dhambi) na itaathirika kutokana na dhambi hii.

Hivyo ili Waislamu waweze kusimamisha Uislamu (Ukhalifa wa Allah) katika jamii, kila Muislamu anasathiki kuufahamu Uislamu vilivyo na pawekwe mazingira ya makusudi yatakayomuwezesha kila Muislamu kujielimisha katika fani maalumu ya maisha inayohitajika katika jamii kwa kadiri ya vipaji alivyoruzukiwa na Mola wake. Kwa maana nyingine kila Muislamu mwenye vipaji vya kuwa Daktari au Mhandisi au Mwanasheria au Mchumi au Mwalimu, n.k ajizatiti kuiendea taaluma hiyo na jamii ijizatiti kumuwezesha.

Endapo, kwa mfano Muislamu mwenye kipaji cha kuwa Daktari, akazembea asiwe Daktari atakuwa mas-uli mbele ya Allah (s.w). Pia endapo jamii ya Waislamu itazembea isitoe Madaktari wanaohitajika itakuwa mas-uli mbele ya Allah (s.w).

## Elimu yenye Manufaa

Elimu yenye manufaa ni ile ambayo: **Kwanza**, humuwezesha mja kufikia lengo la kuumbwa kwake. Tumeona kuwa elimu imekuwa faradhi ya kwanza kwa waumini kwa kuwa elimu ndio nyenzo kuu ya kuwawezesha binaadamu kufikia lengo la kuumbwa kwao ambalo ni kumuabudu Allah (s.w), ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yao. (Qur-an 51:56). Pia elimu ndio nyenzo kuu ya kuwawezesha waumini kuwa viongozi wa jamii (makhalifa wa Allah) katika ardhi. (Qur-an 2:30 - 31).

Elimu itakayotafutwa kinyume na kumuwezesha mtu kumuabudu Mola wake ipasavyo na kusimamisha ukhalifa wa Allah (s.w) katika ardhi itakuwa si elimu yenye manufaa bali elimu yenye kuhasirisha kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Anayetafuta elimu isiyokuwa kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w), hasomi kwa lengo lolote lile ila la kupata maslahi ya hapa duniani tu. Huyo siku ya kiyama hatapata hata harufu ya Pepo." (Ahmad, Abu Daud, Ibn Majah).

Pia Mtume (s.a.w) ametuasa kuwa mwenye kutafuta elimu ili awazidi wasomi wengine au ili kuitumia katika biashara za kijahili au ili kujionesha kwa watu kuwa naye ni msomi, Mwenyezi Mungu atamuingiza motoni. (Tirmidh).
Pili, elimu yenye manufaa kwa binaadamu hapa ulimwenguni na huko akhera ni ile ambayo pamoja na mtu binafsi kuitumia katika kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo katika maisha yake ya kila siku, huifundisha au huifikisha kwa wengine pia kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w).
Ni vibaya mno mbele ya Allah (s.w) mtu kukataa au kuacha kufikisha kwa wengine kila anachokijua kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:
"Abu Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Atakayeulizwa juu ya jambo alilojifunza kisha akaficha (akakataa kutoa elimu ile) atavalishwa mshipi wa moto katika siku ya Kiyama". (Ahmad, Ibn Majah, Tirmidh na Abu Daud). Katika hadith nyingine iliyosimuliwa na Abu Hurairah Mtume (s.a.w) amesema: "Mfano wa elimu isiyonufaisha ni sawa na mfano wa mali iliyokusanywa bila ya kutumiwa katika njia ya Allah". (Ahmad, Darini).

Kutokana na hadith hizi tunajifunza kuwa elimu yenye kunufaisha ni ile iliyofundishwa kwa wengine kinadharia na kiutendaji. Kwa kufundisha watu unachokijua bila ya wewe mwenyewe kutenda ni mfano mbaya mno kwa wale wanaofundisha na chukizo kubwa mno mbele ya Allah (s.a.w): "Enyi mlioamini mbona mnasema msiyoyatenda?) Ni chukizo kubwa mbele ya Allah (s.w) kusema msiyoyatenda." (61:2-3)

*****************************

**JIPIME**

1. Elimu ni nini?

2. "Sema, Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?..." (39:9) Ni kwasababu gani wanaojua hawawi sawa na wasiojuwa?

3. Unatoa maoni gani iwapo wanaojua na wasiojua wakawa sawa kiutendaji?

4. Elimu yenye manufaa kwa binaadamu ni ile................................

5. Eleza sababu tatu zinazopelekea elimu kupewa nafasi ya kwanza katika Uislamu.

## UISLAM UMEMPA HESHIMA MWANAMKE

Uislam umempa mwanamke heshima kubwa, ushahidi ni maneno ya Mwenyezi Mungu aliyetakasika yaliyomo ndani ya Qur'an na Hadithi za Mtume:

Ni sehemu nyingi ametajwa mwanamke kwa heshima ndani ya Qur'an na Hadithi za Mtume (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) ila natoa aya chache na Hadithi kama mfano:-

**Mfano wa aya kuhusu usawa katika kumcha Mwenyezi Mungu**

"Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda." (an-Nahl, 97)

"Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi." (al-Hujurat, 13)

"Na Tumemuusia insani kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameibeba mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa katika miaka mwili; ya kwamba, unishukuru Mimi, na wazazi wako; Kwangu ndio mahali pa kuishia". [Luqmaan: 14].

**Mfano wa Hadithi kuhusu hesima ya mwanamke kama mzazi**

Mtu alikuja kwa Rasuli wa Allaah (Swalla Allaahu alayhi wa salam) na akasema:

"Ee Rasuli wa Allaah! Nani miongoni wa watu wote anastahiki uhusiano wangu wa karibu?" Nabiy akajibu. "Mama yako"

Yule mtu akauliza tena, "kisha nani?" Nabiy akamjibu

"Mama yako"

Yule mtu akauliza tena, "kisha nani?" Nabiy akamjibu

"Mama yako"

Yule mtu akauliza tena, "kisha nani?" Nabiy akamjibu.

"Baba yako"

Kwa hiyo haya yanasisitiza kwamba mama mtu anapewa heshima mara tatu kuliko baba mtu.

Na kuhusu mke, hadhi yake na taathira yake katika kutuliza moyo na kuliwaza imeonyeshwa wazi wazi katika Aayah Tukufu (kauli ya Allaah), katika msemo wake Mtukufu:

"Na katika Aayaat (ishara, dalili) Zake ni kwamba Amekuumbieni katika jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao; na Amekujaalieni baina yenu mapenzi na rahmah. Hakika katika hayo, bila shaka pana Aayah (ishara, zingatio nk) kwa watu wanaotafakari". [Ar-Ruwm :21].

## Mwanamke Mshirika Katika Maisha

Mwenyezi Mungu Mtukufu asema:

"Enyi watu! Hakika tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane. Hakika ahishimiwaye zaidi miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi.." (49:13)

Je dini zimemdhulumu mwanamke? Wako wasemao hivyo lakini kabla ya kujibu swali hili kwanza ni lazima tufafanue mambo mawili:

Lazima tutofautishe kati ya dini zingine na dini ya Kiislam, kwa sababu katika dini zingine mwanamke huenda akawa na picha mbaya. Nami sina shaka kwamba dini iliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu haiwezi kumdhulumu mwanamke au kumvunjia heshima.

Ama katika dini ya Kiislam, mwanamke ana heshima, na anatukuzwa zaidi ya mwanamume.

Ni lazima tutofautishe kati ya mafunzo ya dini kwa mwanadamu na wanaadamu wenyewe wanaoifuata hiyo dini, kwani huenda ikawa hao wanaofuata dini wanamdhulumu mwanamke katika nyanja fulani, lakini hatuwezi kusema hivyo ndivyo dini inavyotaka, kwa sababu dini yenyewe haitaki uonevu, uwe umefanyiwa mwanamume au mwanamke au hata wanyama na mimea. Kwa hivyo mimi ninapozungumzia haki za mwanamke, sizungumzii msimamo wa wafuasi wa dini, bali nazungumzia msimamo wa dini, basi nasema hivi; dini haiwezekani imdhulumu mwanamke, kwa sababu ndogo tu, nayo ni kwamba dini ni MFUMO wa maisha uliyoletwa na mwenyewe aliyeumba hayo maisha. Na ikiwa Mwenyezi Mungu alimuumba mwanamke ili amtukuze, basi amemuumba ili amrehemu, ili amuingize peponi, kama alivyomuumba mwanamume kwa hayo; kwa hivyo haiwezekani amdhulumu, kwa sababu huyo mwanamke hakuchagua awe mwanamke au mwanamume.

Mwanamke huzaliwa mke, hana hiyari, na mwanamume pia huzaliwa mume pasina hiyari. Vipi tena dini imhukumu mwanamke kwa jambo ambalo hakulichagua yeye mwenyewe (la kuwa mwanamke)?

Kwa hakika dini ya Kiislamu yapinga vikali kila aina ya ubaguzi wa jinsi ya mtu alivyozaliwa bila ya kujiamulia mwenyewe. Mathalan ubaguzi wa rangi (mtu hakukhiyari awe mweupe au mweusi), ubaguzi wa lugha, n.k. Dini haibagui mweusi wa Afrika wala mweupe wa Ulaya, wala haibagui kati ya anayezungumza lugha ya Kiingereza au Kijerumani au lugha nyingine. Wala haibagui aliyezaliwa nchi fulani au nyingine, kwa sababu kuchagua rangi, jamii au nchi anayozaliwa mtu hakuko chini ya uwezo wa mtu huyo. Aidha dini haibagui kati ya mume na mke kwa sababu kuchagua jinsi ya kuwa mume au mke hakuko kwenye uwezo wa mwanadamu.

Ama kuhusu kutenda mema dini haibagui katu, hapa yafafanua:

"...Hakika sitapoteza amali ya mtendaji mema miongoni mwenu awe mwanamume au mwanamke." (3:195)

Aya nyingine yafafanua:

"Na watakaofanya mema wakiwa wanaume au wanawake hali wao ni wenye kuamini basi hao wataingia peponi."

(4:124)

Vilevile dini yakwambia kwamba, uwezo wa mtu kujichagulia awe mume au mke uko kwa Mwenyezi Mungu.

"Yeye ameumba namna mbili mume na mke." (53:45)

Na yamkemea vikali anayebagua kati ya mume na mke:

"Na mmoja katika wao anapopewa khabari ya (kuzaliwa kwake) mtoto wa kike uso wake huwa mweusi akajaa sikitiko. Akawa anajificha watu (wasimuone) kwa sababu ya khabari ile mbaya aliyoambiwa! (anawaza) Je akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni (kaburini akiwa hai)? Sikilizeni! Ni mbaya mno hukumu yao hiyo."

(16:58-59)

(Mambo haya yalikuwa yakifanywa wakati wa ujahiliyya kabla ya Uislamu).

Hii ndiyo picha jumla ya mtazamo wa dini juu ya mwanamke. Na sasa hebu tuangalie kwa ufafanuzi dini isemavyo:

Tukiuliza dini, je una maoni gani au kwa maelezo ya ndani zaidi, nini mtazamo wako juu ya mwanamke? Tunaiona hapa dini ikijibu: Mwanamke yu hali tatu:

Mwanamke anapokuwa mdogo na msimamo wa baba yake kwake.

Mwanamke anapoolewa na msimamo wa mumewe kwake.

Mwanamke anapokuwa mama na msimamo wa wanawe kwake.

Katika hali ya kwanza (anapokuwa mdogo) twaona kwamba Uislamu wamwambia babake kupitia kwa Mtume (saw) akisema: "Mtoto wa kike ni rehma na wa kiume ni neema." Mtume (saw) pia amesema: "Bora ya watoto wenu ni mabinti." Amesema pia: "Bora ya watoto ni mabinti wenye kujisitiri."

Imepokewa Hadith nyingine kwamba: Mtume (saw) alipopewa bishara ya kuzaliwa mtoto wa kike, aliwaangalia maswahaba nyusoni akawaona wamechukizwa, akawaambia: “Mna nini nyinyi? Hilo ni ua la rehani ninalolinusa na aliloniruzuku Mwenyezi Mungu.”

Vile vile twaona katika maisha ya Mtume (saw) kwamba yeye hajawahi kubusu mkono wowote ila mikono ya watu wawili tu:

**Mkono wa bintiye Fatima Zahra** alipokuwa na miaka tisa, ilikuwa kila aingiapo kwa babake, alikuwa akisimamiwa na babake (Mtume (saw)) kumbusu mkono wake na akimketisha mahali pake; na hilo alilifanya hasa kwa ajili ya kuwaonyesha na kuwafundisha umma wake kutowabagua watoto wa kike.

**Mkono wa mchapa kazi**, aliyekwenda kwa Mtume (saw) akampa mkono, Mtume (saw) akahisi usugu wa mkono wa mtu yule, akamuuliza, “Mbona hivi?” Yule mtu akajibu: “Huu usugu ni kwa sababu ya kuchapa kazi ee Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Mtume (saw) akainama, akambusu mkono wake huo akasema: “Huu ndiyo mkono unaopendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake!”

Vilevile unahimiza baba anaponunua zawadi za watoto wake, mtoto wa kike apate mbili na wakiume apate moja. Au binti atangulie kupata kabla ya mvulana.

Imepokewa Hadith kutoka kwa Ibni Abbas; Mtume (saw) amesema: “Atakayekwenda sokoni na kununua zawadi akenda nayo kwa familia yake (nyumbani) huyo ni kama aliyechukua sadaka na kuwapelekea wahitaji, basi na aanze kwa kuwapa watoto wa kike kabla ya watoto wa kiume, kwani atakayemfurahisha binti yake ni kama aliyemwacha huru mmoja miongoni mwa wana wa Ismail (as). Na mwenye kumfurahisha mtoto wa kiume, mtu huyo ni kama anayelia kwa kumcha Mwenyezi Mungu.”

Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi humtanguliza mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike katika maneno na vitendo vinavyohusu mambo yote ya nyumbani. Mtu humnunulia mtoto wake wa kiume akamwacha wa kike au anaposhauri, kuhusu mambo ya ndani ya nyumbani kwake humshauri mtoto wake wa kiume na asimshauri wa kike.

Wazazi wengi wanawapa kipaumbele watoto wa kiume na kuwashughulikia sana kuliko watoto wa kike jambo linalowafanya watoto wa kike wajihisi kuwa wanadharauliwa na hilo huwafanya wakawa na chuki. Kufanya hivi, licha ya kuwa haifai kisheria, vilevile huacha athari mbaya kwenye uhusiano wa wavulana na wasichana na hasa pale kila mmoja wao anapokuwa mwenye familia yake mwenyewe. Jambo hilo twaweza kuligundua tunapochunguza zile familia zenye aidha wasichana tu au wavulana pekee; ambapo utaona watoto wataishi wakiwa wameshikamana, ama wanapokuwa chini ya baba yao, ama kila mmoja anapokuwa tayari ana familia yake, kwa sababu watoto hao hawakubaguliwa kijinsia. Lakini kinyume nao, wale watoto walioonja ubaguzi wa kijinsia utawaona hawana mshikamano pale wanapofikia kila mtu wakati wa kujitegemea.

Mtume (saw) asema: “Mtu atakayekuwa na mtoto wa kike na hakumdhalilisha wala hakumtanguliza mwanawe wa kiume zaidi ya huyo wa kike, basi Mwenyezi Mungu atamwingiza peponi.”

Ama hali ya pili: Mwanamke anapokuwa mke wa mtu (rejea nyuma kidogo ili kufahamu zaidi) tutaona kwamba dini ya Kiislamu inamwambia mumewe hivi: “Mcheni Mwenyezi Mungu juu ya wanawake kwani wao ni amana iliyoko kati ya mikono yenu, mmewachukua wao kuwa ni amana ya Mwenyezi Mungu, basi waoneeni huruma na zifurahisheni nyoyo zao mpaka wasimame pamoja nanyi.” Mtume Muhammad (saw).

Vile vile amesema (saw): “Mbora wenu, ni yule aliye mbora kwa mke wake, nami ni mbora kwa wake zangu.”

Anaendelea kusema Mtume (saw): “Mja hatazidi kuwa na imani ila atazidi pia na kuwapenda wanawake (aliowaoa na kuwahurumia wanawake kwa ujumla.)”

Katika Hadith nyingine nyingi asema:

“Mtu atakayemuoa mwanamke basi na amheshimu.”

“Dunia ni starehe, na bora ya starehe za dunia ni mke mwema.”

“Mambo matatu mtu akiyapata amefaulu: mke mtiifu, nyumba yenye nafasi na mnyama mwenye kasi(kipando).”

Katika Hadith nyingine! “Jibril hakuwacha kuniusia kuhusu wanawake mpaka nikadhani itakuwa haram kuwaacha.”

Imam Ali naye asema: “Ama haki za mkeo, ni wewe ujue ya kwamba Mwenyezi Mungu amemjaalia kuwa ni kitulizo na liwazo kwako, na ujue hiyo ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwako”.

## MAISHA YA FAMILIA YA MKE NA MUME

Kwa mtazamo wa dini, mke ni mshirika katika maisha, yeye ndiye anayemkamilisha mume na mume ndiye anayemkamilisha mke. Wewe wamuhitajia, naye pia akuhitajia. Mke si mtumishi, bali ni ‘mke’ kwa hivyo anafaa kutumikiwa.

Ama haki ambazo mwanamke lazima amtekelezee mumewe ni:

**Ya kwanza** ni haki ya kitandani (tendo la ndoa), kumpa mwili wake mumewe anapotaka. Pia Uislamu hapo wasema mtu ajiandae kwa mkewe kama ambavyo mke ajiandae kwa mumewe (kabla ya TENDO ). Mume anapoomba hilo na hali zinaruhusu, basi mke ni lazima awe amejiandaa. Sayyidna Ali (k.w.) amesema: “Mke aliye muovu zaidi ni yule amnyimaye mumewe (tendo la ndoa).”

**Haki ya pili** ni mume kujua mke anapotoka nyumbani, yaani ajue mke anakokwenda. Haifai katika Uislam mke ajiendee tu popote au vyovyote atakavyo wakati mumewe hataki. Mtume (saw) amesema: “Mke yeyote atakayetoka nyumbani kwa mumewe bila ya idhini ya mumewe, basi huyo hulaaniwa na kila kitu kinacho chomozewa na jua na mwezi mpaka mumewe amridhie.” Kwa kuwa anajua sababu iliyomfanya atoke ni nzuri hawezi kumficha mumewe. Na ikiwa mume ni mtu muumini haamrishi wala hakatazi ila kwa sababu ya maana. Basi mke anapotoka bila ya idhini yake kila kitu kitamlaani mpaka mume ajue sababu ya kutoka kwake na aridhike.

**Haki ya tatu** ni kulinda mali za mumewe anapokuwa hayupo na hata akiwepo kwani mali zao wote na siyo kuzitumia kwa fujo au kuziacha zikaharibika bila kusaidia mume wake kuzitunza ikiwa yuko karibu na anaziona mali hizo.

Ama haki za mume kwa mkewe ni nyingi:

Mume amridhishe mkewe katika tendo la ndoa, na kimapenzi na haifai mume aache kabisa kuonana na mkewe kimwili. Haifai asionekane kwa muda mrefu bila ya udhuru wa maana.

Ni juu ya mume amtimizie mkewe mahitaji ya lazima, nyumba inayofaa, mavazi yafaayo na chakula.

Mke si mali ya mume bali ni mshirika wake katika maisha anaingia mkataba na mume kwa ajili ya kuishi pamoja na kupendana pamoja na kule watoto pamoja.

Kwa hivyo, mke si katika majukumu yake kumtumikia mumewe bali ni upendo na ushirikiano. Mume anakalifiwa ki-sheria na kibinaadamu kutosheleza mahitaji yote yanayohitajika.

Ama kupika, kufagia, kufua au kuajiriwa ili kupata pesa, haya yote si wajibu wa mke bali ni hiari na heshima kwa upendo juu ya mume wake.

Mke ni "mke" wala si mtumishi, atakapojitolea kufagia, kupika, kunyonyesha na kulea ni hiari yake kwa upendo wa mume wake na familia wala si lazima katika dini bali ni ihsan na wema.

Akijitolea naye mume asimpatilize mathalan kwa kuzidi kutia chumvi kwenye chakula au maji si baridi, nyumba chafu au haikusafishwa vizuri. Kwa sababu hawajibiki na hayo yote, madhali amejitolea basi afanye ni hisani kwa mume. Na kwa sababu hii ndipo tunakuta historia yasema kwamba Mtume (saw) hakulaumu katu mapishi ya chakula katika maisha yake. Alikuwa akishirikiana na wakeze kupika na kufagia na akisema: "Wale wafanyao kazi nyumbani mwao ndio wa kweli katika umma wangu."

Ama hali ya tatu ya mwanamke ni pale anapokuwa mama, uislamu unawalazimisha watoto kumheshimu, inasema Qur'an.

"Wala usiwaambie Ah!…" (17:23)

Hapo juu tumesoma Hadithi hii:

Kijana mmoja alikwenda kwa Mtume (saw) akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni yupi aliye bora zaidi kwangu nimtendee mama?" Mtume akamjibu: "mamako." Yule kijana akauliza "kisha nani?" Mtume akajibu: "kisha mamako." Akuliza tena: "Kisha nani?" Akajibu: "Kisha mamako" akauliza (mara ya nne): "Kisha nani?" Akamjibu: "Kisha babako".

Yaani hii ni kuonyesha kwamba haki za mama ni nyingi zaidi kuliko za baba mara tatu zaidi.

Alikwenda kijana mwingine kwa Imam Sadiq (A.S) akasema: "Ee mjukuu wa Mtume, mimi nilimbeba mama yangu mgongoni kwangu na kuhiji naye mara nyingi akiwa mgongoni kutoka Madina hadi Makka, je nimetekeleza haki zake?" Akatabasamu Imam Sadiq akamjibu: "Wallahi bado hujatekeleza haki yake hata ya usiku mmoja alipoamka akakuwekea titi lake mdomoni ukanyonya."

Hivi ndivyo ilivyo, utaona kwamba Uislamu unaangalia mwanamke kama mwanaadamu aliyeumbwa na Mungu kwa matakwa haswa ya muumba, kama alivyoumba mwanamume kwa kutoka kwake yeye muumba na ndio maana akaamrisha mwanamke ahishimiwe.

Anapokuwa msichana, dini yakwambia mheshimu. Anapoolewa, dini yakwambia mheshimu, na anapokuwa mama, dini yakwambia mheshimu.

Dini inawatahadharisha wale wanaowapiga wake zao, inasema: “Mwenye kunyoosha mkono wake ili amzabe kofi mwanamke huyo ni kama aliyeunyoosha mkono wake motoni.”

Pili inasema: “Mkeo asiwe ni mtu umchukiaye, kwa kuwa mwanamke ni ua la mrehani si mtumishi. Na jiepusheni na wivu pasipo mahali pake, kwani kufanya hivyo humfanya yule mzima akapata maradhi, na asiye na hatia kumtia kwenye shaka.”

## MTAZAMO WA KIJAMII JUU YA MWANAMKE WA KIISLAM

Baadhi ya watu hujiuliza kuhusu Hijab, kwa nini dini ikawajibisha? Wengine huuliza: Je inafaa mwanamke afanye biashara, au ukulima?

Wengine wanataka kujua je mahari ni thamani (bei) ya mwanamke? Na wengine wanauliza kama inafaa mwanamke mmoja aolewe na waume wengi!

**Ama kuhusu Hijab**, kwa hakika mtazamo wa dini kwa mwanamke ni mtazamo wa kijumla, yaani ujumla mwanamke ni binaadamu na siyo wa kujistarehesha naye tu.

Kwa hivyo inatubidi tumuangalie ki-upande huo, lakini kwa kuwa yeye ni kivutio kwa sababu ana maumbile mazuri ya kike yanayomvutia mwanamume, ndipo dini ikafaradhisha Hijab ili kuzuia mwanamke asigeuzwe njia ya kujistarehesha, na haifai tumtazame mwanamke kama bidhaa ya kuuzwa au chombo cha starehe kama yanavyofanya maendeleo ya ki-magharibi ambayo yamemvua ubinadamu wake na kumbakishia uanamke wake ndipo akafanywa ni kitu cha matangazo ya biashara ili kumvutia mteja. Mwanamke anatumika kwenye biashara kiasi kwamba wanapotaka kuuza gari humsimamisha msichana mzuri kando ya gari hilo wakampiga picha nalo ili lipate kuuzwa.

Isitoshe hata wanapotaka kuuza farasi maalum, watamsimamisha msichana mrembo kando ya ranchi ya farasi ili awavutie wanunuzi wamnunue farasi huyo. Hata kwenye matangazo ya bustani ya kufugwa wanyama mwanamke amekuwa akitumika! Hivi ndivyo mwanamke anavyotumika kwa faida ya kibinadamu naye huhitajiwa tu pale anapokuwa mrembo wa kumezewa mate; ama akiwa havutii au ameumbwa na uzuri wa kawaida tu, huwa hana thamani kwa sababu huyo hawezi kuvutia wanaume.

Ama Uislamu haukubali mwanamke atupwe kwenye matamanio, kama alivyosema Imam Ali: “Mwanamke ni rehani na si mtumishi.” Mrehani lazima uhifadhiwe. Na mwanamke ni almasi lazima athaminiwe. Tunaposema almasi lazima ifichwe ili isiibiwe, je huko utasema ni kuivunjia heshima almasi au kuichunga? Basi vivyo hivyo mwanamke na Hijab!

Hapana. Hijab si kumtweza mwanamke bali ni kumchunga kutokana na wizi wa wenye matamanio ya kingono kwa kuona maungo na maumbile. Na maadam mwanamke anatakiwa na mwanamume kwa matamanio basi yampasa ajihifadhi maumbile yake ya kike kwa njia inayofaa, nayo ni kuficha vivutio vyake. Mwanamke mzuri ni yule anayejistiri mwili wake na waume wengine na kujionyesha kwa mumewe tu. Mtume (saw) asema: “Bora ya wanawake zenu ni yule mzazi, mwenye mapenzi, mwenye kujisitiri, mwenye kumtii mumewe, mwenye kujichunga na mwingine, anayemsikiliza na kumtii amri zake na wanapokuwa faragha, humpa akitakacho.”

Amesema pia: "Mbora wa wanawake wenu ni yule anapokuwa faragha na mumewe huvua vazi la kuona haya."

Ama kuhusu wanaume ambao hawamtaki ila kwa ajili ya kufaidi tu, Uislamu umemzuia na hilo. Kwa sababu kijana anayemchukulia msichana kama mpita njia tu kwa ukweli huwa hana haja naye ila hutaka kutimiza haja za matamanio yake tu wala hana penzi. Kwa hivyo anachotaka ni kukidhi haja zake tu wala hajali mabaya wala mazuri ya mwanamke huyo.

Mara ngapi tumeona matukio kadha wa kadha katika nchi mbalimbali ambapo msichana amechukuliwa na kijana akatembea naye kisha akamwacha abebe mateso yake.

## KAZI NA BIASHARA KWA MWANAMKE WA KIISLAM

**Kuhusu kufanya kazi**, Uislamu haumkatazi mwanamke kufanya kazi yoyote. Uislamu hausemi kwamba ni haramu kwa mwamanke awe mfanyi kazi au mkulima au mfanyi biashara, bali ni haki ya mwanamke afanye kama afanyavyo mwanamume katika kufanya kazi, kulima, biashara n.k. kwa sharti tu awe na "heshima" na kuulinda utu wake.

Uislamu unakataza kwenda tupu na mwanamke kujionyesha sehemu za mwili wake, haukatazi kufanya kazi.

### Bi Khadija bint Khuwailid(R.A) Alikuwa Mfanya Biashara

Sote tunajua ya kwamba Bi Khadija bint Khuwailid (r.a.) alikuwa tajiri na mfanya biashara mkubwa na alijuana na Mtume (saw) kupitia biashara zake ambapo Mtume (saw) alikuwa akifanya kazi kwake.

Mwanamke anaweza kufanya kazi ikiwa atahifadhi Hijab yake kazini, au asichanganyike na wanaume wawezao kumuoa. Kwa sababu bila ya kufanya hivyo atageuka kuwa ni burudani kwa wanaume.

**Ama kuhusu mahari**, kwa mtazamo wa uislamu, ni alama ya kuonyesha kuwa msichana huyu anatakiwa na mvulana huyu. Hutolewa mahari ili mwanamke ajihisi kuwa anahitajiwa na mwanamume na si yeye anayemtaka mume, jambo linalo mtosheleza haya zake alizoumbwa nazo na heshima zake ambazo bila shaka zitavunjika pale yeye atakapomtaka mwanamume.

Mahari si thamani ya bei anayolipa mume kuununua mwili wa mwanamke, na ndipo ukaona uislamu haukupanga kiwango cha mahari na kitu chochote chaweza kuwa mahari (k.v. vyombo n.k.) hata kumfundisha hesabu au sura ya Qur'an kunaweza kuwa mahari, au chochote hata kiwe kidogo namna gani.

Isitoshe, uislamu unapenda mahari yawe kidogo. Mtume (saw) anasema: "Bora ya wanawake wa umma wangu ni wale wazuri wa uso wenye kutolewa mahari kidogo." Na kila mahari yanapokuwa kidogo, inaamanisha kwamba huyo msichana (kwani ndiye anayetaja mahari) anamtaka huyo mume mwenyewe na si mali yake, na huyo mume anamtaka mke mwenyewe si kwa sababu amemnunua.

Kuhusu suala la mke na waume wengi, dini imekataza hilo kwa sababu hizi:

Mwanamke hafai kushea ikiwa wewe hufai kushea hata kalamu yako, utaridhika kushirikana mkeo?

Suala la kuona ni utangulizi wa kupata watoto, na kuwa na waume wengi ni kuchanganya watoto.

Mwanamke ana hisia za 'ulinzi' yeye vyoyote ilivyo anatafuta mtu wa kumlinda. Hebu uliza nchi gani inayotawaliwa na maraisi wawili? Au dola gani ya ndoa inayotawaliwa na waume wawili?

Hata upande wa mume kuoa wake wengi wasizidi wanne uliuhusiwa na uislamu kwa sababu ya kutatua matatizo mengi, ikiwa ni pamoja na idadi ya wanawake kuwa kubwa zaidi ya wanaume. Nchini Marekani pekee, kuna wajane milioni tisa waliofiwa na waume zao, na mamilioni ya washichana ambao hawajaolewa.

Vilevile sababu ya kuwa na wake wengi yaweza kuwa ni kwa ajili ya maslahi ya mwanamke kwa mfano; hebu tuchukulie mke ni tasa, hazai na mumewe anataka watoto na kisha mume tumzuie asiwe na wake wawili (asioe), hii ina maana kwamba tutamruhusu amuache yule mkewe ili aoe wa pili. Hii kwa kweli itakuwa si kwa maslahi ya yule mkewe.

Hili ndilo suala la mwanamke, ambaye ana heshima yake katika uislamu, kwa sababu yeye ni kiumbe cha Mungu, na amejaaliwa hivyo na Mungu muumba kwa ajili ya kujuana kama isemavyo Qur'an:

"Enyi watu! Hakika tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane. Hakika ahishimiwaye zaidi miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi.." (49:13)

Ama maendeleo ya kimagharibi (Ulaya) heshima ya mwanamke imevunjwa, amekuwa ni thamani tu ya kibiashara au burudani ya ki-ngono mambo yanayoutweza utu wake na hili sisi hatuliridhii wala hatutaki limpate mwanamke.

Siku moja Mtume (saw) alikuwa ameketi na baadhi ya maswahaba zake kwenye changarawe akachora kwa kidole chake ardhini mstari ulionyooka, kisha kando ya msitari huo akachora msitari ya mshazari, mmoja upande wa kulia na mmoja wa kushoto, akaashiria kwenye ule msitari wa kwanza ulionyooka akasema: "Hii ni njia ya Mwenyezi Mungu, kisha akaashiria kwenye ile mistari mingine akisema: "Na hizi ni njia zingine ambazo juu ya kila njia pana shetani anayewaita watu waifuate. Kisha akafumba macho kwa muda mfupi kidogo, kisha akasema: "Kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka, basi ifuateni. Wala msifuate njia zingine mtafarikiana na njia ya Mwenyezi Mungu."

Kwa hivyo hapa Mtume ameeleza upotofu wa kila njia isiyolingana na njia ya Mungu kama vile alivyoonyesha jinsi njia ya Mungu inavyojitenga kimsingi na njia za shetani. Sasa basi, tunapotaka kuigundua njia ya Mungu kuhusu masuala ya mwanamke tusiwaulize mashetani, na maana ya mashetani hapa ni wote walioanguka chini ya matamanio. Yatupasa tuangalie kwenye maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume, kwa sababu mapenzi ya nafsi daima hufikiria lile jambo ilitakalo na hayafikirii ukweli ulivyo.

Mtu akisema 'Hijab hakuna katika uislamu' wakati yeye anasoma jinsi Qur'an inavyosema kuhusu hijabu ya kuvaa na kuhusu kutochanganyikana mfano aya hii "…na mnapowauliza kitu basi waulizeni nyuma ya pazia (hijab), mtu huyo hakusudii hijab kama ilivyo kwenye uislamu ila ni kwa kuwa hijab haikuridhisha matakwa yake ya kimwili ndiyo maana akasema hakuna hijab.

Hivyo ndivyo ilivyo, na kwa hakika uislamu ndio unaopanga njia ya Mwenyezi Mungu na si watu wengine, na ndipo hapa tunakuta kwamba Mwenyezi Mungu anaweka orodha ndefu kuhusiana na maswala ya mwanamke:

Maisha ya mwanamke ya kipekee

Masuala ya mwanamke ya kijamii

Masuala ya mwanamke ya kifamilia

Masuala ya mwanamke ya ki-jinsia.

Ufafanuzi wa masuala haya ni kama ifuatavyo:

Kuhusu masuala ya muhusuyo ni kwamba yeye anapaswa kutenda yale yapasayo mwanamume kuyatenda kama kufanya ibada, kuwa na tabia nzuri n.k.

Mwanamke ana haki zote za kijamii na anaweza kufanya biashara kulima na kufanya kazi mradi tu ahifadhi heshima yake ya kike.

## WAJIBU WA MWANAMKE NDANI YA FAMILIA

Kifamilia, mwanamke ni msimamizi wa utekelezaji ndani ya nyumba ambapo mume anakuwa ni kiongozi wa taasisi ya familia. Aya isemayo: "Wanaume ni wasimamizi wa wanawake" haimaanishi mwanamume atumie mabavu, na kulazimisha mambo; uislamu haumuangalii mwanamke kama mtumishi au mnyonge au asiye na mawazo ya kushauri lolote ndani ya taasisi ya familia.

Mwanamke ni mshirika wa mwanaume, si mtumishi kwa hivyo yampasa mume kwa sababu mke ni msaidizi na mwanamume ni kiongozi wa familia amuandalie mshirika wake huyo maisha mema ya ki-binaadamu.

Yampasa mke aishi vizuri na mumewe na amtosheleze na starehe za jinsia inavyotakiwa na kwa ndoa ya kisheria, na uislamu una utaratibu na miongozo juu ya suala hili linalofafanua kwa usawa kwa mume na mke njia za kukutana kimwili , nayo ni miongozo iliyofafanuliwa inayoeleza hata namna ya kufanya tendo la ndoa na wakati muwafaka wa hilo.

Kwenye orodha hizi zinazohusu masuala ya mwanamke katika uislamu tunagundua kwamba zinamuangalia mwanamke kuwa ni mwanaadamu, mwenye haki ya kuishi kwa usawa na mwanamume.

Mwanamke si bidha ya kutumika na kustarehesha wenye matamanio tu na kuacha aende zake matamanio yanapomalizika, mwanamke ana heshima na kuthaminiwa kama msaidizi wa mume ndani ya taasisi ya familia.

Na kama tulivyoona, ni kwamba Uislamu unafanya juhudi kuona kwamba umedhibiti starehe za kimwili kwenye familia na maisha ya ndoa. Uislamu hauruhusu starehe hizo kutangazwa sokoni, barabarani, mabarazani au kwenye mikusanyiko. Pia hauruhusu kwenda uchi, kujionyesha mapambo, au kuchanganyika kuovu kwa wake na waume na kukaa faragha. Hayo yote yanaambatanishwa na adabu, desturi na hukumu maalum.

Hivi ndivyo Uislamu unavyolipa suala la mwanamke la jinsia picha yake halisi na kulipa umuhimu kama yalivyo masuala mengine yawe ya kijamii au ya kifamilia. Hivyo ndipo uzani wa usawa unapohifadhika na kuzuia mwanamke asitumiwe kama chombo cha madhambi au kisanamu cha kuchezewa.

Ama mifano mingine (isiyo ya Kiislamu) yenye misingi na hukmu ambayo inaendelea hivi leo chini ya kivuli cha 'maendeleo inafanya juhudi za kufanya mwanamke awe ni 'jinsi

nyingine'. Asipotimiza wayatakayo basi hapana haja awepo. Kwa msingi hii haya yote yamepangwa juu ya desturi za mambo hayo, ambapo baadaye hakuna kizuizi kwa mwanamke kuyafuata kama; kusambaratika kwa familia, kuzaa nje ya ndoa, kuenea zinaa n.k.

Kwa hivyo mwanaadamu leo yampasa achague moja kati ya njia mbili. Ama njia ya kujizuia, (maisha ya ki-familia ya ndoa) au njia ya zinaa (kuharibika kwa familia).

Njia ya kwanza ni ya Mungu na ya pili ni ya shetani. Wale wanaochagua njia ya pili, yawapasa wafahamu kwamba jambo haliishi kwa wao kuifuata kando kando (bora wasifuate kabisa). Ama kujaribu kuchanganya baina ya njia mbili hakufai ila ufuate njia ya Mungu tu. Kwa sababu njia ya shetani ni njia ya matamanio nayo hayana mwisho mwema. Kila mwanaadamu anapotopea humo, matamanio nayo humwambia; vipi nyongeza!

## MAJUKUMU YA MWANAMKE KIMAISHA

Si sahihi mwanamke abebeshwe majukumu asiyoweza kuyabeba. Hata sayansi inatuonyesha kimsingi jinsi mwanamke alivyo tofauti na mwanamume.

Dkt. Casius Carel, mshindi wa tuzo la Nobel katika sayansi anasema: "Mambo yanayomtofautisha mwanamume na mwanamke hayaishii kwenye maumbile ya viungo vyao vya uzazi tu, au tofauti katika malezi yao tu, bali kuna mambo mengi. Tofauti hizo zina maumbile ya kimsingi zinazoanzia kwenye mpangilio wa kimwili, mwanamke katika kila kiungo cha mwili wake ana vitu vya maji maji vya kemikali vinavyorutubisha uzao. Wale wanaodai kuwa na malezi sawa, elimu na kazi baina ya wanaume na wanawake hawazijui tofauti hizi kabisa; tofauti za kimsingi. Mwanamke alivyo hasa ana tofauti kubwa na mwanamume kwani kila chembe chembe (cell) katika mwili wake ina umbile la kike, hata mpangilio wa mishipa yake uko tofauti."

Anaendelea Dkt Carel: "Utaratibu na kazi za vuingo vya mwili una mpangilio maalum kama vile elimu ya nyota na hesabu. Haiwezekani kufanya badiliko lolote kwa kuwa tu mwanaadamu anataka kubadilisha. Kwa hivyo letu sisi ni kukubali kama ilivyo. Na wanawake nao ni lazima wakuze vipawa vyao kulingana na maumbile yao, na waache kuwaiga wanaume kiholela. Nafasi yao katika maendeleo ni kubwa kuliko ya mwanamume na haifai kuiacha."

Maadam majaribio ya kisayansi yameonyesha tofauti hizo za kimaumbile, basi yapasa kutenganisha suala la mwanamume na la mwanamke. Kila mmoja wao apewe wadhifa ule utakaolingana na sifa zake. Mwanamke ana sifa za huruma basi ni lazima kazi ya kulea watoto aachiwe yeye, kwa sababu kazi hiyo inahitajia huruma. Na mwanamume kwa kuwa ana nguvu za kubeba majukumu mazito, basi hapana budi apewe uongozi wa kusimamia nyumba na nchi.

Isitoshe, inapasa ratiba ya masomo ya mwanamke ibadilishwe ili iambatane na tabia, umbile na akili yake.

Vilevile hapana budi majukumu yake katika maisha ili yalingane na shakhsiya yake ya huruma.

Tutakapomweka mwanamke kwenye nafasi yake ifaayo basi tutaweza kuinua hali ya nchi iliyoporomoka. Kwani kumpa kila mtu nafasi yake anayohusika nayo ndiko kumwezesha kupata fursa kwenye jamii ya kufikia maendeleo.

Jamii ya mwanadamu ina mfumo wa “kutofautiana”. Ama jamii ya wanyama ina mfumo wa “kuwa sawa”. “Kutofautiana” ina maana ni kutofautiana watu na kila aliye na sifa fulani kumfanyia na kumkamilishia mwingine ambapo “kuwa sawa” maana yake ni kuwa sawa bila ya kushughulikiana. Kwa hivyo hapa, utaona kuwa mwanamume anamuhitajia sana mwanamke na mwanamke anamuhitajia sana mwanamume. Lau ingelikuwa mwanamume na mwanamke “wako sawa”, basi mmoja asingelimuhitajia mwengine.

Dkt. Maranon anasema: “Jambo linalothibiti ni kwamba, ukamilifu wa mwanadamu utatimia, na lazima utimie, kwa kuziainisha tofauti zao, yaani mwanamume ajione zaidi ni mwanamume, na mwanamke ajione zaidi kuwa ni mwanamke.”

Kwa hivyo ni upumbavu wanawake wawaige wanaume, na wanaume nao kuwaiga wanawake.

Msichana aliye baleghe hapendezi mbele ya mwanamume pale anapovaa Mini au Kaptula (Short pants) kama vile mwanamume avae gauni, viatu vya mchuchumio (High heels) pochi kwapani na ajitie manukato ya kike.

Takwimu zimeonyesha kwamba wanaume hupendelea sana wanawake wenye kujiheshimu kuliko wenye kujidhihirisha wazi wazi. Ndiyo, ni kweli mvulana (mhuni) mhuni hupata kumchezea msichana anayevaa Mini anapompitia mbele yake barabarani.

Lakini penzi liko mbali na suala la ndoa ya daima, kwani mwanamume katu hawezi kumuoa msichana mwenda-uchi. Anajua wanawe atakaozaa naye wataharibika kwa sababu mama atakayewalea atapenda zaidi kujipamba kwa ajili ya wanaume wengine ili awavutie, kuliko kuwalea wanawe.

Na msichana apendaye kuangaliwa na maelfu ya macho yenye njaa naye hajaolewa, basi hata atakapoolewa atapenda zaidi macho ya watu yamuangalie. Haitaishia hapo, mwisho itafikia kupokea wanaume watakampigia miluzi na kumfuatilia kwa ahadi za uongo ili wakidhi kiu ya uchu wao wa ngono nje ya ndoa na kisha wamkimbie na kumtangaza kwenye jamii .

Familia nyingi zimesambaratika kwa sababu mwanamke si mwenye kujistahi. Kwa kweli ni ujinga wa mwisho mwanamke avunje heshima yake kwa sababu tu watu maarufu wanakwenda uchi na  wanafanya hayo anayoona ndio maendeleo, au vijana wajifanye kama watu mashuhuri wa wasio na staha wafanyavyo? Kuwa mashuhuru si kuwa kiigizo bali kiigizo ni tabia njema inayoendana na mafunzo ya dini sahihi ya uislam kwa kumridhisha Muumba wa pekee na si kuwaridhisha walimwengu.

## CHAKULA NA LISHE

Chakula na lishe bora ni muhimu kwa binadamu wote. Chakula ni kitu chochote kinacholiwa na kuupatia mwili virutubishi; ambapo lishe ni sayansi ya jinsi mwili unavyokitumia chakula. Lishe inahusisha jinsi mwili unavyosaga na unavyoyeyusha chakula na hatimaye virutubishi kusharabiwa (kufyonzwa) na kutumika mwilini.

### Faida za chakula kwa binadamu:

- Kutengeneza seli za mwili na kurudishia seli zilizokufa au kuharibika
- Ukuaji wa akili na mwili
- Kuupa mwili nguvu, joto na uwezo wa kufanya kazi
- Kuupa mwili kinga dhidi ya maradhi mbalimbali.

Ulaji bora ambao unazingatia chakula mchanganyiko na cha kutosha ni muhimu kwa

binadamu wote, na ni muhimu zaidi kwa wagonjwa.

Inasisitizwa kula chakula mchanganyiko na cha kutosha mara zote kwani hakuna chakula kimoja pekee ambacho kinaweza kumpatia binadamu mahitaji yake yote ya kilishe isipokuwa maziwa ya mama tu kwa mtoto katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo.
Inasisitizwa kula chakula mchanganyiko na cha kutosha mara zote kwani hakuna chakula kimoja pekee ambacho kinaweza kumpatia binadamu mahitaji yake yote ya kilishe isipokuwa maziwa ya mama tu kwa mtoto katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo.

## Virutubishi, umuhimu na vyanzo vyake

Virutubishi ni viini vya kikemia vilivyoko kwenye vyakula ambavyo mwili hutumia ili kufanya kazi mbalimbali. Karibu vyakula vyote vina virutubishi zaidi ya kimoja ila kwa kiasi tofauti. Vyakula vingine huwa na virutubishi vya aina fulani kwa wingi zaidi.
Kila kirutubishi kina kazi yake katika mwili wa binadamu, na vingi hutegemeana ili kufanya kazi vizuri mwilini.

Zifuatazo ni aina za virutubishi:

- Kabohaidreti
- Protini
- Mafuta
- Vitamini
- Madini

## Kabohaidreti

Hiki ni kirutubishi muhimu kwa kuupa mwili nishati (nguvu) kwa ajili ya kufanya kazi mbalimbali pamoja na joto. Kabohaidreti ndio inayochukua sehemu kubwa ya mlo.
Kabohaidreti inajumuisha wanga, sukari na nyuzinyuzi.
Vyakula vyenye kabohaidreti kwa wingi ni pamoja na mahindi, mchele, uwele, ngano, viazi vya aina zote, mihogo, ndizi, sukari na baadhi ya matunda. Nyuzinyuzi ni muhimu sana katika uyeyushwaji wa chakula.



## Protini

Protini ni muhimu sana kwa ukuaji wa mwili na akili. Protini husaidia mwili kutengeneza seli mpya, kutengeneza vimeng’enyo mbalimbali na wakati mwingine

protini huupa mwili nishati kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Baadhi ya vyanzo vizuri vya protini ni aina zote za nyama, samaki, aina za mikunde kama choroko, kunde,maharagwe, soya, karanga, pia maziwa, mayai, dagaa na wadudu wa aina mbalimbali wanaoliwa kama senene, n.k.



## Mafuta

Mafuta huhitajika mwilini kwa ajili ya kuupa mwili nguvu na joto pamoja na kusaidia usharabu wa baadhi ya vitamini. Mafuta pia hulainisha chakula na kukifanya kiwe na ladha nzuri, na hivyo kumfanya mlaji ale chakula cha kutosha.

Mafuta hupatikana kwa wingi kwenye samli, siagi, baadhi ya nyama, baadhi ya samaki, mbegu zitoazo mafuta kama ufuta, korosho, mbegu za maboga, karanga, alizeti, mbegu za pamba, kweme,mawese pamoja na nazi.



## Vitamini

Vitamini zinahitajika mwilini kwa ajili ya kulinda mwili pamoja na kuufanya mwili ufanye kazi zake za umetaboli vizuri. Vitamini ziko za aina nyingi na zinapatikana kwa

wingi kwenye mboga-mboga, matunda na kwenye vyakula vinavyotokana na wanyama kama maziwa, aina zote za nyama, mayai, dagaa, samaki, n.k.



## Madini

Madini kama ilivyo vitamini hulinda mwili na kuufanya ufanye kazi zake za umetaboli vizuri. Kuna aina nyingi za madini, na baadhi ya vyakula vyenye madini kwa wingi ni pamoja na vyakula vinavyotokana na wanyama, dagaa, samaki, mboga-mboga na matunda.

KUMBUKA

Vyakula huwa na kirutubishi zaidi ya kimoja, hivyo vyakula vinavyotajwa kwenye kirutubishi fulani humaanisha vyakula hivyo vina kirutubishi hicho kwa wingi.

**Makundi ya vyakula na mlo kamili**

Pamoja na kuzungumzia virutubishi mbalimbali, ni muhimu kukumbuka kwamba mtu anapokula hafikirii virutubishi bali chakula. Hivyo ni muhimu katika kujifunza ulaji bora, kutumia makundi ya vyakula badala ya aina za virutubishi. Pia ni muhimu kukumbuka kwamba vyakula vingi vina virutubishi zaidi ya kimoja, na pia kiasi hutofautiana.



Kwa afya na lishe bora, inashauriwa kula mlo kamili (chakula mchanganyiko). Mlo kamili hutokana na vyakula ambavyo vimewekwa pamoja kwa namna ambayo vikiliwa pamoja huupatia mwili virutubishi vyote muhimu kwa afya bora. Hutayarishwa kutokana na mchanganyiko wa angalau chakula kimoja kutoka katika kila kundi, katika makundi yafuatayo:

## Vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi:

Vyakula hivi ndivyo vinavyochukua sehemu kubwa ya mlo na kwa kawaida ndiyo

vyakula vikuu. Vyakula katika kundi hili ni pamoja na mahindi, mchele, mtama, ulezi, ngano, uwele, viazi vikuu, viazi vitamu, mihogo, magimbi, viazi mviringo na ndizi.

- **Vyakula vya mikunde na vyenye asili ya wanyama:**

Vyakula vilivyoko katika kundi hili ni pamoja na maharagwe, njegere, kunde, karanga, soya, njugu mawe, dengu, choroko na fiwi. Vile vyenye asili ya wanyama ni pamoja na nyama, samaki, dagaa, maziwa, mayai, jibini, maini, figo, senene, nzige, na wadudu wengine wanaoliwa.

- **Mboga-mboga:**

Kundi hili linajumuisha aina zote za mboga za majani zinazoliwa, zile zinazolimwa na zinazoota zenyewe. Mboga-mboga ni pamoja na mchicha, majani ya maboga, kisamvu, majani ya kunde, matembele, spinachi, mnafu, mchunga, pia aina nyingine za mboga kama karoti, pilipili hoho, biringanya, matango, maboga, nyanya chungu na bamia, bitiruti, kabichi na figiri.



**Matunda:**

Kundi hili linajumuisha matunda ya aina zote kama mapapai, maembe, mapera, malimau, mapesheni, mananasi, peasi, machungwa, machenza, zambarau, mafenesi, mastafeli, parachichi, tango,n.k . Aidha "matunda pori" yana ubora sawa na matunda mengine. Matunda hayo ni kama ubuyu, ukwaju, embe, n.k.



- **Mafuta na sukari:**

Mafuta na sukari ni muhimu ingawa vinahitajika kwa kiasi kidogo mwilini. Mafuta yanaweza kupatikana kutoka kwenye mimea kama mbegu za alizeti, ufuta, karanga, mawese, mbegu za pamba n.k na kutoka kwa wanyama kama siagi, samli na nyama ya mafuta. Sukari inapatikana kwenye sukari, miwa, asali na vyakula ambavyo vinatengenezwa kwa sukari nyingi kama jamu.

***Kumbuka;***

## Maji

Maji kwa kawaida hayahesabiwi kama kundi la chakula, lakini yana umuhimu mkubwa katika afya na lishe ya binadamu.

Inapaswa kunywa maji ya kutosha, angalau lita moja na nusu (glasi nane) kwa siku au hata zaidi. Inashauriwa kunywa maji zaidi wakati wa joto kali ili kuzuia upungufu wa maji mwilini.
Vilevile unaweza kuongeza maji mwilini kwa kunywa vinywaji kama supu, madafu, juisi za matunda mbalimbali.



Mtu anatakiwa kula mchanganyiko wa vyakula kwenye mlo mmoja kwa sababu hakuna chakula kimoja chenye virutubishi vyote muhimu kwa ajili ya lishe na afya bora. Vilevile baadhi ya virutubishi hutegemeana ili kuweza kufanikisha kazi zake mwilini. Kwa mfano madini ya chuma yanayopatikana kwenye vyakula vya mimea kama mboga-mboga za kijani husharabiwa vizuri mwilini kama kuna vitamini C ambayo hupatikana kwa wingi kwenye matunda. Mfano mwingine ni zile vitamini kama A, D, E, K ambazo usharabu na utumikaji wake mwilini hutegemea kuwepo

kwa mafuta. Vilevile nishati huweza kutumika vizuri mwilini iwapo kuna aina za vitamini B kwenye vyakula.

HIVYO;
Kwa mtu yeyote ni muhimu kula mlo ulio kamili angalau mara mbili au tatu kwa siku na asusa (vitafunwa) kati ya mlo mmoja na mwingine.

KUMBUKA
Katika jamii zetu, matumizi ya mboga-mboga na matunda yamesahaulika sana. Inabidi kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha kwamba mboga-mboga na matunda vinakuwa sehemu ya mlo.

## VITAFUNWA VYEPESI

## POP CORN NA KARANGA





## VITAFUNWA ASILIA

Unaweza kuchemsha Viazi vitamu, mihogo, ndizi mbivu, magimbi, maharagwe na ukanywa kwa chai, hii ni bora kifya

### MIHOGO YA KUCHEMSHA NA SAMAKI WA KUKAANGA



MAHITAJI/INGREDIENTS

*1.Mihogo Vipande 12*
*2.Samaki*
*3.Maji Nusu Lita*
*4.Chumvi wastani*
*5.Mafuta ya kupikia Kikombe 1*
*7.Pilipili ukipenda*
*8.Kachumbari*
*9.Ndimu Vijiko Vya Chakula 4*
*10.Vitunguu thaumu Punje 3*

MAANDALIZI/PREPARATIONS

*1.Osha samaki vizuri baada ya kuwasafisha kisha waweke kwenye bakuli*

*2.Twanga kitunguu thomu na pilipili na chumvi*

*3.Weka viungo ulivyotwangwa kwenye samaki*

*4.Ongeza ndimu kisha wachanganye vizuri*

*5.Menya mihogo na ikoshe vizuri*

*7.Kata mihogo kupata vipande 12*

**JINSI YA KUPIKA/HOW TO COOK**
**MUHOGO/CASSAVA**

*1.Weka mihogo kwenye sufuria pamoja na maji na chumvi*

*2.Chemsha hadi mihogo iwive na kuwa laini*

*3.Mwaga maji yaliobakia kwenye mihogo na iwe mikavu*

*4.Weka mihogo kwenye sahani*

**SAMAKI WA KUKAANGA**

*1.Weka mafuta kwenye kikaangio*

*2.Weka kikaangio jikoni weka moto mkali*

*3.Baada ya dakika 3 weka samaki*

*4.Baada ya dakika 5 wageuze samaki upande wa pili*

*5.Waache kwa dakika 5 nyengine*

*6.Toa samaki wako waweke kwenye tissue au chujio wachuje mafuta*

*7.Baada ya dakika 3 wako tayari kuliwa*

*8.Kula samaki na mihogo pamoja na kachumbari  na pilipili*

*9.Unaweza kula na chai au uji ukipenda*




## JINSI YA KUPIKA CHAPATI LAINI

**MAANDALIZI**

*1.Kwanza hakikisha unakanda unga vizuri*
*2.Lazima unga uukande mpaka uwe laini sana*
*3.Baada ya kukata madonge ya idadi ya chapati unazo zitaka*
*4.Wakati wa kusukuma tumia unga kuhakikisha unapata duara kubwa kiasi*
*5.Yeyusha samli au blue band changanya na mafuta kupaka katika duara lako*
*6.Kunja unavyopenda ila kumbuka jinsi unavyo ikunja ndio inatengeneza muonekano mzuri wa chapati*
*7.Baada ya kuziweka mafuta ni vizuri uziache kiasi cha dakika 10 mpaka 15 kabla ya kuzipika*
*8.Sukuma chapati jitahidi upate duara zuri lenye shape ya kuvutia*
*9.Unapo sukuma chapati isiwe nyembamba wala nene sana iwe na upana wa kiasi*
*10.Chapati ikiwa nyembamba sana unapo ichoma huwa ina kakamaa na ikiwa nene sana huwa haiivi vizuri inaweza kuwa mbichi*

**JINSI YA KUPIKA**

*1.Moto hapa ndio kwenye mambo yote ukikosea chapati nayo inaweza kuwa mbaya*
*2.Moto ukiwa mdogo hupelekea chapati kunyonya mafuta*
*3.Moto ukiwa mwingi chapati huungua*
*4.Weka moto wa wastani ili uivishe chapati yako taratibu*
*5.Weka chuma jikoni pakaa mafuta kijiko kimoja*
*6.Weka chapati yako jikoni*
*7.Iache kidogo sana yaani ikisha kubadilika kutoka ubichi tu geuza upande wa pili*
*8.Acha iive mpaka ianze kufanya rangi za kuiva*
*9.Usiache mpaka ikaungua*
*10.Izungushe zungushe kwenye chuma ili sehemu zote zipate ile rangi ya kuiva hasa nchani mwa chapati*
*11.Ikunje sehemu mbili sawa*
*12.Weka mafuta kijiko kimoja*
*13.Penyeza kijiko kati kati ya chapati*
*14.Fanya kama unaigandamiza huku ukiisugua na chuma*
*15.Ongeza mafuta kidogo izungushe chapati hadi upate rangi nzuri ya kuvutia*
*16.Geuza upande wa pili rudia hatua ya 13 mpaka 16*
*17.Ikunjue irudi kuwa duara*
*18.Acha ule upande wa nyuma ya chapati uive kidogo tu*
*19.Itoe malizia kuchoma chapati zilizobakia kwa hatua hizo ziliopo juu*
*20.Njia hii ya upishi wa chapati hupelekea chapati kuchambuka wakati wa kuipika chapati*

***Angalizo:Note***

*1.Ukikosea kukanda unga na kuwa mgumu na hizi njia za chini zote zitakataa kutoa chapati laini*
*2.Ni vizuri kupika upishi huu ukiwa huna haraka taratibu kupata chapati nzuri*
*3.Ni upishi unaohitaji mazoezi pika mara kwa mara hadi utaziweza*



## Maandazi ya Mayai na Maziwa

Maandazi ni moja ya kitafunwa maarufu sana Tanzania. Pika maandazi na uweze kufungua kinywa kwa maandazi ya mayai na maziwa. Haya maandazi yanaweza kunywewa chai, juice na pia kahawa.

Mahitaji

- Unga wa ngano ½ kilo
- Sukari 200g (kikombe kimoja cha chai)
- Chumvi ½ kijiko kidogo (cha chai )
- Hamira kijiko 1 kidogo
- Yai 1
- Maziwa ya unga vijiko 2 vikubwa
- Butter kijiko 1 kikubwa
- Hiliki kijiko1 kidogo
- Maji ya uvuguvugu ya kukandia
- Mafuta ya kuchomea lita 1
- Kibao cha kusukumia unga wa ngano
- Sinia au ubao ulionyooka

Maelekezo

- Weka unga kwenye bakuli kisha ongeza sukari, chumvi, yai, maziwa ya unga, butter na hiliki. Changanya viambato mpaka mchanganyiko uwe sawia.
- Ongeza maji ya uvuguvugu kiasi kwenye mchanganyiko na uanze kukanda. Ni vizuri kukanda mchanyiko huu kwa muda wa dakika 15 ili kuhakikisha donge lote la unga limelainika vizuri.
- Gawanya unga uliokwandwa katika madonge manne (4) tofauti.
- Weka unga wa ngano kidogo katika kibao cha kusukumia na uanze kusukuma donge moja katika shape ya chapati. Katika kusukuma, hakikisha unga wako uko wa wastani – siyo mwembamba sana wala mnene.
- Ukimaliza kusukuma kata unga kutokana na umbo upendalo kupika maandazi na uyatandaze katika ubao au sinia lililonyooka. Hakikisha sinia au ubao umenyunyuziwa unga wa ngano ili kuzuia unga utakaoweka usingandie.
- Rudia hiyo hatua kwa madonge yote yaliyobakia.
- Ukimaliza kuandaa maandazi yako, weka maandazi yako katika sehemu iliyokuwa na joto ili yaweze kuumuka. Hii inaweza kuchukua hadi masaa 3 ili hamira kuumua vizuri unga wako.
- Unga ukishaumuka, bandika sufuria, au kikaangio pamoja na mafuta jikoni. Hakikisha mafuta ni mengi ili kuwezesha maandazi kuiva vizuri.
- Mafuta yakishachemka tumbukiza mandazi. Acha maandazi kwenye mafuta mpaka yabadilike rangi na kuwa ya brown.
- Maandazi yakishaiva, ipua na weka kwenye chujio ili kukausha mafuta. Rudia hatua hizi kwa maandazi yote yaliyobaki.
- Subiri yapoe na yako tayari kuliwa.

## Mkate wa maboga, nazi, na maziwa



Wote tunapenda vitamu. Huu mkate una mchanganyiko wa virutubisho vyenye kukupa afya. Kizuri zaidi ni rahisi kuandaa na gharama yake ni nafuu. Unachohitaji ni jiko lako (si lazima oven) na viambato vingine. Vanilla inaipa hii scones harufu tamu, maziwa na tui la nazi vinakupa vionjo vya kukufanya utamani kula zaidi. Unaweza kula scones hizi kwa chai, kahawa au kula pamoja na vinywaji tofauti baridi.

Mahitaji

- Unga wa ngano Kilo 1
- Hamira kijiko 1 cha chakula
- Chumvi 1/2 kijiko cha chai
- Sukari kijiko 1 kidogo cha chai
- Maziwa  au tui bubu la nazi (Au vyote kwa pamoja)
- Uji mzito wa maboga ya njano yaliyochemshwa na kupoa kikombe kimoja cha chai (Siyo lazima)
- Vanila 1/2 kijiko kidogo cha chai
- Siagi kidogo.

Maelekezo

- Andaa maji ya uvuguvugu ujazo wa nusu kikombe kidogo cha chai.
- Weka hamira kwenye ya maji ya uvuguvugu kisha funika kwa muda wa dakika 3 hadi 5
- Andaa unga wa ngano. Chekecha ili kutoa uchafu ( kama una mchanyiko na vitu tofauti)
- Pasha moto sufuria ya kukandia
- Chemsha mafuta ya kula (mililita 20 – 30)
- Mimina hamira ( iliyoumuka kwenye maji) kwenye unga. Changanya vizuri kisha mimina mchanganyiko kwenye mafuta yanayochemka.
- Koroga kwa kutumia mwiko, japokuwa ni vizuri sana ukitumia mkono ( kuwa makini mafuta yasiwe ya moto sana)
- Ongeza maziwa au tui la nazi na endelea kukanda hadi unga uwe laini na usigandiane na sufuria
- Weka siagi kidogo kisha endelea kukanda.
- Weka vanilla kisha endelea kukanda. Vanilla inaleta harufu nzuri kwenye scones zako.
- Ukimaliza kukanda vizuri, paka sufuria mafuta, weka mchanganyiko wa unga uliokanda kisha funika na weka sehemu yenye uvuguvugu au joto kwa dakika 30 -45 ili unga uumuke vizuri. Joto liwe kati ya nyuzi 80°C hadi 120°C. Kama unatumia Oven ni vizuri kama utawasha ili lipate moto kabla ya kuweka mchanganyiko wa unga. Zima kabla ya kuweka mchanganyiko wako. Kisha weka mchanganyiko ili uumuke vizuri. *Si lazima oven, unaweza kutumia jiko la mkaa lenye moto mdogo kiasi au jiko tofauti kwa kurekebisha kiwango cha joto.*
- Mchanganyiko wa unga wenye hamira ukishaumuka vizuri, kanda tena kiasi na kisha gawa matonge madogo madogo (kutokana na umbo utakalo). Panga matonge kwenye mduara wa sufuria ambao umepaka mafuta (siagi) kisha weka kwenye sehemu yenye joto au vuguvugu kwa muda dakika 45. Joto liwe kati ya nyuzi 80°C hadi 120°C.
- Angalia kama unga umeumuka vizuri na kuongezeka kwenye sufuria. Weka moto kwenye jiko la mkaa ili liwe la moto kwa dakika 10 . Punguza moto na injika sufuria yenye scones juu ya jiko. Palia mkaa wenye jivu la moto juu ya mfuniko na subiri kwa dakika 10 kisha funua uangalie kama zimeiva. Kama bado ongeza moto wa jivu kidogo na subiri kwa dakika 5 zaidi.
- Ukifunua na kuona zimebadilika rangi na kuwa kahawia ( brown) zipake siagi kwa juu na funika. Baada ya dakika 2 mimina scones zako kwenye chombo kisafi na acha zipoe.
- Unaweza kula na scones hizi kwa chai, maziwa, kahawa, vinywaji tofauti. Ni njia mbadala ya kuwapikia watoto wakiwa wanaenda shule ili kuweza kula wakati wa mapumziko, vilevile ni kitafunwa kizuri kwa wale wanaoenda kazini na hawana muda wa kula nyumbani.



## Kebab za nyama

Unaweza kuandaa kebab hizi kwa kutumia nyama ya samaki, kuku au ya ngombe. Kebab hizi zinaweza kuliwa kama kiambato cha chakula kikuu, lakini pia unaweza kula kama kitoweo kwa vinywaji tofauti – ni ubunifu wako tu.

Mahitaji

- Fillet za nyama ya ng'ombe, kuku au samaki (Tuna)
- Yai 1
- Slice ya mkate 1
- Pilipili hoho 1
- Kitunguu maji 1
- Kitunguu saumu 1
- Karafuu iliyosagwa
- Chumvi
- Limao
- Coriander

Maelekezo

- Andaa vitunguu – pilipili hoho, kitunguu saumu na kitunguu maji – menya na kata vipande vidogo. Ponda kitunguu saumu kwenye kinu.
- Andaa nyama (samaki, kuku au ya ng'ombe) kwa kuikata vipande, kuiosha na kisha kuichemsha.
- Weka ndimu na chumvi kwenye nyama.
- Nyunyuzia pilipili manga
- Usiongeze maji kwenye nyama. Acha ikauke.
- Nyama ikikauka, weka kitunguu.
- Loweka slice ya mkate kwenye maji. Itoe na ikamue kisha changanya na mayai lililopasuliwa na kukorogwa PAMOJA VIZURI. Hakikisha mchanganyiko umejichanganya vizuri.
- Injika kikaangio jikoni. Weka mafuta mengi kiasi. Subiria yachemke.
- Tengeneza umbo la uviringo kutoka kwenye nyama,samaki au kuku kisha chovya kwenye rojo la mkate na mayai
- Tumbukiza mchanganyiko kwenye mafuta. Ingiza kimoja baada ya kingine. Ili kupata matokeo mazuri, ingiza kwenye mafuta, huku ukitumia mshikio, weka mchanganyiko ndani ya mafuta kwa muda wa sekunde 5 – 8 ili kujenga koti na kuwezesha kuiva vizuri.
- Rudia hatua hii kwa vipande vyote vilivyobaki.
- Ipua vile vilivyoiva na subiria vikauke – unaweza kula.



## Karanga za mayai

Karanga za mayai ni nzuri maana zinatupatia virutubisho vingi muhimu. Unaweza kula kwa kimiminika chochote au ukala zenyewe na ukazifurahia.

Mahitaji

- Karanga kilo 1
- Yai moja
- Mafuta ya kula ( ya maji ) mls 750
- Sukari vijiko 6 vya chakula
- Unga wa ngano kikombe kimoja cha kahawa( coffee cup)
- Chumvi ya unga nusu kijiko cha chai.
- Jiko
- Chombo –Sufuria/bakuli
- Mwiko /kijiko kikubwa

Maelekezo

- Chukua yai, pasua na koroga kwenye chombo kisafi.
- Chukua karanga,mimina kwenye chombo ulicho koroga yai ,changanya kwa kutumia mikono.
- Weka chumvikidogo, changanya vizuri, weka sukari changanya, mimina unga wa ngano, changanyavizuri.
- Weka mafuta jikoni hadi yapate moto.
- Chota karanga kwa kutumia kijiko kikubwa na weka kwenye mafuta kisha zigeuze bila kuacha hadi utakapoona karanga zimebadilika rangi kua kahawia.
- Tumia kijiko kikubwa kuziepua na weka kwenye chombo kisafi cha wazi ilizipoe.
- Funga kwenye vifuko vidogo na zihifadhi mahali pasafi tayari kwa kula au kuuza.



## Sambusa za nyama

Sambusa za nyama hupendwa na watu wengi mana ni tamu, unaweza kula kwa soda, juice au chai, pia waweza kula zenyewe tu na ukafurahi

Mahitaji

- Nyama steki kilo 1
- Vitunguu maji 2
- Majani ya Giligiliani vifungu 2
- Garam masala kijiko 1 cha chai
- Chumvi kijiko 1 cha chai
- Pilipili manga kikijo 1 cha chakula
- Kitunguu saumu kilichosagwa kijiko 1 cha chai
- Tangawizi ya Unga kijiko 1 cha chai
- Karoti 2 kubwa
- Pilipili hoho 2
- Unga wa ngano vijiko 4 vya chakula au ute wa yai
- Manda
- Butter kijiko kimoja cha chakula

Maelekezo

- Bandika nyama weka chumvi, mpaka iive iwe laini. Hamisha supu pembeni ibaki nyama tu.
- Chukua mashine ya kusagia nyama, weka giligilia kwenye nyama, anza kusaga nyama na giligiliani pamoja, funika weka pembeni.
- Kata kata vitunguu maji, muundo wa box size ndogo sana, kata karoti na pilipili hoho. Weka pembeni.
- Chukua frying pan pana, weka butter. Ikianza kuchemka weka vitunguu maji, karoti na pilipili hoho, koroga visiive.
- Weka kitunguu saumu kilichosagwa, weka pilipili manga na tangawizi koroga vizuri.
- Weka nyama, koroga vizuri ili ichanganyikane na viungo vingine, weka garam masala koroga dakika 2, epua. Usiifunike
- Koroga unga wa ngano au ute wa yai, hii itakusaidia kufungia sambusa.
- Chukua manda, kata kwa umbo la pembetatu. Kisha weka nyama kiasi, anza kufunga ila ukifika mwisho paka ute wa yai au unga wa ngano uliokoroga.
- Inasaidia sambusa zisifunguke wakati wa kupika.
- Bandika mafuta yakipata moto anza kupika,mpaka uone sambusa zimegeuka rangi na kua kahawia. Epua anza kula na familia au peleka kuuza.



## Kashata za nazi

Mahitaji

- Sukari kikombe 1
- Nazi kikombe 1
- Mdalasini wa kusaga nusu kijiko cha chai
- Cardamon nusu kijiko cha chai
- Maziwa vijiko 2 vya chakula
- Unga wa ngano (option)
- Rangi ( option)

Maelekezo

- Pasua nazi, toa ile nyama ya ndani weka kwenye blender, weka na maziwa saga mpaka iwe laini sana. Au unaweza kukuna kwa kutumia kibao cha mbuzi.
- Washa moto, bandika sufuria jikoni likipata moto weka sukari, koroga mara kwa mara mpaka iyeyuke na kua brown.
- Punguza moto, weka nazi, mdalasini, cardamon, rangi, unga koroga vizuri kwa dakika 2 ili mchanganyiko uchanganyikane.
- Chukua sinia lipake mafuta, toa mchanganyiko ule jikoni umwage kwenye sinia chukua kijiko, usambaze uenee vizuri.
- Uache upoe kwa muda.
- Kata saizi unayotaka ukiwa bado wa moto, ukimaliza uache upoe kisha kula na familia na unaweza kuuza ukipenda.

## UJASIRIAMALI NA UCHUMI





Katika ulimwengu wa sasa ambao ajira zimekuwa ngumu na shida kupatikana, ujasiriamali na biashara vimekuwa ndio kimbilio la wengi. Watu wengi wanaingia kwenye biashara kama njia kuu ya kujipatia kipato.

Pamoja na biashara kuonekana kuwa kimbilio la wengi sio wote wanaoingia kwenye biashara wanafanikiwa. Tafiti zinaonesha kwamba asilimia tisini ya biashara zinazoanzishwa zinakufa mwaka mmoja baada ya kuanzishwa. Na hata hizo zinazovuka mwaka mmoja asilimia tisini hufa baada ya miaka mitano.

## Dhana ya uchumi katika uisilam




Uisilam umekemea uvivu wa kazi. Kazi halali ni ibada yenye malipo. Kwa watu wote ambao wametimia kiroho, kiakili na kimwili bado hawatumii vyema neema hizi kwa kiwango cha juu kuhakikisha makundi mengine yanahudumiwa vyema katika matumizi ya uchumi unaotokana na wao waliotimia wanakuwa wanafanya makosa. Makundi kama ya wazee wasio na uwezo, yatima, makundi ya wajane wasiojiweza na kila kundi ambalo linastahili kupata msaada wa kiutu yafaa kuhudumiwa na walio na neema hizo.
Uisilam ni mfumo kamili wa maisha. Kwa kutambua maana ya UCHUMI hapo juu, lazima utambue kuwa upatikanaji wa rasimali zote ambao unapelekea huo uchumi kujengeka , umepewa maelekezo yake na Allah (S.W).

Maelekezo yenyewe yamefafanua kwa uwazi;

i. Vipi unatakiwa kuchuma mali yako. Misingi  halali inatakiwa
ii. Vipi unatakiwa kutumia mali uliyoichuma bila kusahau au kudharau haki za chumo la mali uliyopata (kutoa sadaka, zakkah na panapobidi kutoa wakfu).

Mwenyezi Mungu humjaalia baraka tele yule mtu aliyetoa sadaka kwa ajili yake hata kama ni kiasi alichotoa ni kidogo mno. Qur an tukufu inasema;

**"Mfano wa wanaotumia mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano mfano wa punje iliyochipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia,Mmwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua" (Qur an 2: 261).**

Aya nyingine ya Qur an tukufu inasema;
**"Waambie waja wangu walioamini, wasimamishe sala na watoe katika tulivyowaruzuku, kwa siri na dhahiri, kabla haijafika siku isiyo na biashara wala urafiki "(Qur an 14: 31)**

Katika hali halisi, kila kitu ni miliki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwanadamu amepewa haki ya muda tu ya kumiliki. Ndiyo maana mojawapo ya masharti ya kuwa waumini wa kweli ni kuishi tukijua kwamba vitu vyetu vyote tunavyomiliki ni AMANA tu tulivyokabidhiwa. Kwa hali hii, kutumikia mali zetu nje ya mipaka ya sababu mahsusi ni

uvunjaji wa haki ya amana. Siyo tu kwamba adhabu ya matumizi mabaya itakuwa kali huko Akhera, lakini ni dhahiri pia kuwa itasababisha migogoro katika ngazi zote mbili za mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.
Kwa ufupi sana, uwiano wa uchumaji mali na matumizi ya mali katika uisilamu umejengewa misingi moja kwa moja na Allah (S.W) na kwa mafundisho ya Mtume wetu Muhammad (S.W). Maana yake ni kwamba tunayoyashuhudia leo kuwa hali kwenda kombo kwa uwiano wa rasilimali kutokidhi mahitaji kwa jamii kwa uwiano maana yake ni kuachwa kwa mafundisho ya Allah na Mtume kutekelezwa kwa ukamilifu kwake. Mfano kutokuwepo kwa mfumo wa kukusanya zaka na mfumo wa kuzigawa zaka.

Madhara ya kutokutoa katika njia ya Allah ni ni makubwa sana, na si tu kwa Uislamu na Wahitaji, bali pia kwa wale waliowezeshwa na Allah kisha wakafanya ubakhili katika kuwasaidia wahitaji;

**"Na miongoni mwao wapo walio muahidi Mwenyezi Mungu kwa kusema: Akitupa katika fadhila yake hapana shaka tutatoa sadaka, na tutakuwa katika watendao mema. Alipo wapa katika fadhila yake wakaifanyia ubakhili na wakageuka, na huku wakipuuza. Basi akawalipa unaafiki kuutia nyoyoni mwao mpaka Siku watapo kutana naye, kwa sababu ya kuwa walimkhalifu Mwenyezi Mungu katika yale waliyo muahidi, na kwa sababu ya kusema kwao uwongo." (Quran, 9:75-77)**




**"Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubakhili. Na anaye fanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi." (Quran, 47:38)**

## BIASHA NA HALI HALISI YA KIBIASHARA

### Kwa nini biashara nyingi zinashindwa kudumu?

Biashara nyingi zinakufa kutokana na ukosefu wa elimu muhimu kuhusiana na biashara na ujasiriamali. Watu wengi wanaoingia kwenye biashara wanaingia kwa kuangalia tu ni kitu gani watu wengine wanafanya na wao kufanya hivyo hivyo.

Biashara ni rahisi sana kufanya ila ni ngumu kuendesha na kuikuza mpaka iweze kukupa faida kubwa sana. Ili uweze kuendesha na kukuza biashara itakayokupa faida kubwa ni muhimu kuchukua muda na kujifunza vitu vya muhimu vinavyohusiana na biashara.

## BIASHARA NA MATUMIZI SAHIHI YA MUDA

Mfanyabishara au mjasiriamali asiyeweza kutunza muda vyema lazima atakwama tu katika mipango yake. Muda ni rasilimali adimu sana. MUDA NI MALI. Kwa nukta chache hizo hapo juu utatambua kuwa kama hauna hulka nzuri katika kupangilia muda utawezaje kuendesha biashara kubwa na kuwa na mafanikio. Ni wakati sasa wakati tunachambua hizi rasilimali kwa lengo la kujenga uchumi wetu basi tusiwe wenye kulalamika wakati muda mwingi hatufanyi kazi kwa kujibidiisha na tunakaa kupiga porojo zenye kukata tamaa huku tukisubiri kufanikiwa.

Kama kuna muda wa kuwahi katika gulio la mauzo, ukiwa ni mtu wa kupoteza muda bila kujali unadhani unaweza kupata  bidhaa za kununua au utakuta wateja wa kuwauzia bidhaa zako.?
Kwa ufupi MUDA kwa mfanyabiashara ni wa muhimu sana katika mapana yake. Misimu ya mauzo hutofautiana kwa aina ya matukio. Kipindi cha mfungo tatu watu wanauza wanyama wa kuchinja kwa bei ya juu na wanahitajika sana. Mfanyabiasra lazima awe macho na muda wake.

Swala la muda ni swala la mtu binafsi lazima aanze kulitafakari yeye binafsi kwa sababu atakufa na atakutana na Allah ALIYETAKASIKA na ataulizwa muda wake alivyoutumia duniani.
Kwa kutumia mafunzo ya moduli hii muda unatakiwa kuangaliwa kama rasilimali katika taasisi kwa sababu lazima watu wajue wanapokuwa pamoja wasipotezeane muda, lazima wajengeane pepo. Hakuna maana ya kuwa katika taasisi ambayo watu wake kila siku wanapoteza muda wa kufanya mambo kwa wakati. Ni kipindi cha watu kuelezeana sana namna ya kutunza muda. MUDA NI MALI (TIME IS MONEY).




### Maana ya kutunza muda (Time management)

Kutunza muda ni jinsi unavyoratibu na kupanga muda gani utatumia kwa shughuli maalumu.
Kwa hali hii ni vyema mtu akajikita katika kujifunza namna ya kutunza muda kuliko kuutumia huo muda kiholela bila kuwa na umakini. Kuna faida nyingi za kutunza muda, kama zifuatazo;

i. Kuleta tija kubwa na ufanisi katika kazi (Greater productivity and efficiency)
ii. Kujenga haiba kubwa ya ustaarabu (A better professional reputation)
iii. Kufanya mambo kwa raha mustarehe bila kuwa na khofu (Less stress)
iv. Fursa kubwa kwa maendeleo (Increased opportunities for advancement)

Kushindwa kutunza muda ipasavyo juna matokeo mabaya kama yafuatayo;

i. Kukosa kufikia tarehe za ukomo (Missed deadlines)
ii. Kudhorota kwa kazi (Inefficient work flow)
iii. Kazi kuwa na kiwango kibovu (Poor work quality)
iv. Weledi mbovu na taswira mbaya inajengeka
v. Kuwa na khofu kwa kazi za zima moto (Higher stress levels)

## UJASIRIAMALI NI NINI?

Ujasiriamali ni uwezo wa mtu kuona, kugundua, kuvumbua fursa mbali mbali za kiuchumi na kuziongezea ubunifu ama thamani kwa kuziwekea utofauti kisha kuthubutu na kuzifanya fursa kwa lengo la kutengeneza faida/kipato.

## MWANZO WA UJASIRIAMALI:

1) Wazo mahususi(specific idea), linalo kidhi mahitaji ya jamii(linatatua matatizo ya jamii)
2) Utafiti (ukubwa wa soko na bei"market share", tabia za wateja, kipato cha wateja namna ya uzalishaji, gharama za uzalishaji, washindani, sehemu ya biashara "location")
3) Malengo na Mipango (plan) (jinsi ya kuzalisha, wakati, mahali, kupata soko, kupanga bei, kukuza mradi)
4) Mchanganuo: ni taarifa zote zinazo hususiana na mradi zinaweza kuwa nzuri au mbaya).
5) Mtaji (watu, fedha, ujuzi, umaarufu)
6) Weka ubunifu (innovation) utofauti (katika) masoko, wazo, ufungashaji, wakati wa uzalishaji).
7) Mwanzo wa mradi.

## SIFA ZA MRADI WA KIJASIRIAMALI.

A) Ni endelevu kwa kuwa na mipango na mfumo wa utawala ulio wazi (anakufa mmiliki na si mradi).
B) Unatatua matatizo / changamoto za jamii.
C) Unatumia rasirimali chache (watu, mtaji, ardhi,muda) na una faida kubwa kwa mapema au mara kwa mara.
D) Unasoko kubwa na ushindani mdogo kutokana na ubunifu, wakati wa uzalishaji au sehemu)

## MJASIRIAMALI MZURI (mambo ya kuzingatia)

1) Elimu rasmi na siyo rasmi juu ya mradi.
2) Ujuzi wa mambo na utumiaji wa elimu uliyoipata ama uliyo nayo.
3) Huruka ya kupata mafanikio halali. (uthubutu, ubunifu, mvumilivu na jasiri, wepesi wa kuona au kuiga, jitahidi kufanya kazi kwa faida na jitume)
4) Kujiwekea malengo kila hatua, anashaurika na anabeba majukumu,
5) Nidhamu ya kazi, fedha, rasirimali, kuipenda kazi yake.
6) Hakimbii changamoto.
7) Anatunza kumbu kumbu
8) Kupata taarifa za mradi kila inapo bidi na kufanya tathimini.
9) Amechochewa au mwenye vichocheo vya kuendelea kiuchumi kwa kutafuta njia mpya za kujikwamua au kufanya jambo.

## MISINGI YA UJASIRIAMALI.

1) Elimu ya ujasiriamali na kujifunza, kujifunza mambo tofauti ya miradi yake.
2) Ubunifu na uvumbuzi, kuingiza bidhaa mpya katika soko na zinazo kidhi matakwa ya jamii.
3) Kukua na kupanuka, kuwa na mipango ya kuendeleza au kukuza biashara yake kiutawala, bidhaa, huduma au uzalishaji.
4) Kujaribu na kudhamiria, si mwoga wa kutumia fursa anayo iona.

Kabla ya kuanzisha mradi au kubuni wazo la biashara unapashwa kujiandaa kiakili na hisia kuzifuata ndoto zake na kuifanya kazi atakayo ipenda, kujivunia na kuweza kuizungumzia mbele ya jamii.

## MAONO (VISION)

**Nini?**

matarajio yako baada ya kutekeleza wazo/mradi wako (future plan).

## (MISSION)

**Sababu ya kufanya mradi huo na si mingine (statement of purpose) lazima ionyeshe kutatua tatizo au kutumia fursa iliyopo.**

## MALENGO

**Ni mambo unayotaka kuyafikia au kuyapata pia unaweza kuweka na wakati.**

## MFUMO WA MALENGO.

1) Mahususi (specific)
2) Yanapimika (measurable)
3) Yanafikika na changamoto zake (attainable and challangable)
3) Uhalisia (realistic)
4) Muda maalumu (time frame)

## FAIDA ZA UJASIRIAMALI

1. Ujira binafsi na nafasi za ajira kwa watu wengi
2. Kupunguza umasikini miongoni mwa watu
3. Kutumia ipasavyo rasilimali tulizonazo
4. Matumizi sahihi ya rasilimali watu
5. Ujasiamali hutupa mwanga katika kufanya na kuanzisha shughuri mpya
6. Kukuza na kuendeleza uchumi katika nchi
7. Kupunguza kiwango cha umasikini miongoni mwa watu
8. Kupunguza tofauti katika maendeleo baina ya watu, mikoa, nchi n.k

## MJASIRIAMAJI ANAJENGWAJE

## FULSA

Fulsa ni kama uti wa mgongo kwa mjasiliamali. mjasiliamali lazima awe na uwezo wa kutambua au kugundua fulsa, uwezo wa kuchambua na kuchanganua fulsa pia kuchukua hatua juu ya fulsa husika.

## MTAJI

ni kitu chochote ambacho mjasiliamali anawezatumia katika kuzalishia au kufanyia jambo flani kwa lengo la kupata faida. mtaji umegawanyika katika miundo ifuatayo:- mtaji wa fedha,nguvu kazi,mtaji jamii,elimu na utaalamu katika jambo flani.

## UBUNIFU

Kwa kawaida mjasiliamali anatakiwa kuwa mbunifu, ubunifu ndio unamtofautisha mtu mmoja na mwingine hata kama wote watafanya jambo linalo fanana. kilasiku unatakiwa kufikili ni jinsi gani utafanya jambo jipya ua jambo lililofanya na wengine lakini wewe ufanye katika njia tofauti.

## MAWASILIANO

Mawasiliano huunganisha vitu pamoja ana huweka watu pamoja na husaidia kupata taarifu huhimu katika biashara yako.Mawasiliana huunganisha mtaji, fulsa na ubunifu, mjasiliamali anatakiwa kuboresha mawasiliano ili afanikiwe katika ujasiliamali wake.

## JE UNAWEZA KUWA MJASIRIAMALI

Mambo mengi sana yanasemwa, yamesemwa na yataendelea kusemwa kuhusu ujasiriamali na wajasiriamali. Wengi wamefanikiwa. Wamepita katika changamoto nyingi lakini hawakukata tamaa. Wengine, mafanikio yao yamebadilisha dunia kabisa na majina ya biashara zao ndio umekuwa wimbo katika midomo ya watu wengi.

Biashara za wajasiriamali , tena zilizofanikiwa, zimeanzishwa na wajasiriamali wa kila aina. Kila mtu ana hadithi yake na njia yake. Sio kwamba wote wamepita katika njia moja. Hapana! Wapo waliosoma sana, wapo ambao hawajasoma sana na wapo ambao wamesoma kidogo sana. Wengine hawakumaliza shule zao, bali waliishia katikati. Wengine walisoma kwa kiwango kikubwa kabisa. Lakini wote hawa, pasipo kutegemea walikotoka, ni wajasiriamali waliofanikiwa. Wote waliziona fursa, wakazichangamkia na sasa wamefanikiwa.

Baadhi ya wajasiriamali wamekuja na mawazo makubwa kabisa na ubunifu mwingi hata kuanzisha miradi, shughuli na biashara ambazo zimebadili jamii kabisa. Wapo ambao hugundua fursa baada kufanya utafiti wa kina katika mambo, wakitafakali kwa kina wachukue hatua gani sahihi na hata wakihusisha wataalamu mbalimbali katika kuwasaidia.

Lakini pia wapo wajasiriamali ambao wanapopata wazo la biashara , wanalirukia, wanakwenda nalo kama lilivyo na mambo mengine yatajijua mbele ya safari.

Mtu yeyote yule anaweza akafanikiwa katika biashara kama mjasiriamali. Hakuna sifa ya aina moja ambayo ndiyo kama kanuni inayotakiwa ili mtu afanikiwe kama mjasiriamali.

Je ni nini kinakuzuia usifanye ujasiriamali na kuwa mjasiriamali aliyefanikiwa? Endelea kutembelea tovuti ya mjasiriamali.co.tz maana **unaweza kuwa mjasiriamali!**

## AINA ZA UZALISHAJI MALI/BIASHARA

Unaweza kuanzisha biashara kutegemea na uwezo wako kimtaji na mazingira unayomudu bila kusahau ujuzi na uzoefu wa biashara. Kama huna ujuzi na uzoefu basi pata maarifa kwa kuangalia na kujifunza kwa wenye ujuzi ya biashara unayotaka kufanya.

Kuna biashara ya kuuza bidhaa kama nafaka, nguo, spices, n.k
Kuna biashara ya kutoa huduma kama elimu, usukaji, upambaji, matibabu, n.k
Kuna biashara ya uzalisha kama viwanda, kilimo, ufugaji, n.k
Kuna biashara ya uwekezaji kama viwanda vikubwa, majengo ya upangishaji, mitambo ya uzalishaji, n.k

## BIASHARA ZA MTAJI MDOGO ZENYE FAIDA KUBWA

Tuangalie biashara za mtaji mdogo usiozidi Tshs. 100,000 unazoweza kufanya na zenye faida kubwa. Mtaji mkubwa unaohitajika unapoanzisha biashara ni muda na wala sio pesa kama utakavyojifunza hapa.

Mimi binafsi siamini kama kuna biashara ndogo, ila najua kuna biashara unaweza kuanza na mtaji mdogo na zikakuletea faida kubwa.

Hiyo ambayo inaitwa "biashara ndogo" ukiifanya kwa ubora wa hali ya juu na bidii ipo siku itakutoa.

Kabla hatujaenda kwenye hiyo orodha ya hizo bishara za mtaji mdogo, ningependa kuweka sawa maana yangu ninaposema "zenye faida kubwa".
Faida kubwa haimaanishi mamilioni ya fedha, bali ni kwamba faida utakayoipata kulingana na mtaji wako ni nzuri na usipokata tamaa zitakufikisha mbali.

**Zingatia:** Unapotaka kuanzisha biashara yoyote ile, ni vyema kufuatilia utaratibu na sheria za mahali ulipo. Tafadhali ilinde biashara yako kwa kufuata kanuni zote zilizowekwa na serikali.
Orodha ya biashara za mtaji mdogo kama zifuatazo;

### 1. KUNUNUA NA KUUZA BIDHAA

Sifa kubwa ya mjasiriamali ni kuona thamani ya vitu kabla wengine hawajaviona.
Hivyo, tafuta bidhaa ambazo zinauzwa kwa bei ya chini, zinunue na utafute soko ambalo hizo bidhaa zinauzwa kwa bei ya juu uende ukaziuze huko.
Mfano, unaweza kutoa bidhaa Dar es Salaam ukaja kuuza Zanzibar na ukatoa Zanzibar ukauza mikoa mingine.

### 2. KUPIKA KWA ODA

Kama wewe ni mpishi mzuri au una mtu anayejua kupika, basi jitangaze kama unapokea oda za mapishi fulani.Tuchukulie unaweza kupika makande au wali nyama vizuri.
Unachoweza kufanya ni kwenda maofisi ya karibu yako na kuwaambia kwamba wakutafute wanapohitaji hicho chakula wakati wa mchana na wewe utawaletea.
Usisahau kuacha mawasiliano yako ili waweze kukutafuta.
Wengi wao watapenda hiyo huduma kwasababu hawatohitaji kutoka tena kufata chakula.

### 3. KUUZA JUISI NA ICE CREAM

Kujifunza kutengeneza juisi au ice cream haitakuchukuwa muda mrefu, ili kufanikiwa katika biashara hii, cha muhimu ni kujitofautisha.
Muhimu zaidi unapofanya biashara ya kutengeneza juisi au icecream, ni kuweka mazingira yako safi na salama kwa wateja wako. Uzuri wa biashara hii ni kuwa mtaji wake ni mdogo sana.

### 4. KILIMO CHA MBOGAMBOGA

Kilimo ni sehemu kubwa ya maisha ya watanzania na wale wa nchi nyingi za Afrika.
Kila siku zikienda, kilimo huzidi kuwa ni biashara ya matajiri kwasababu shamba lina gharama kubwa.
Licha ya hivyo, bado kuna fursa ya kutengeneza kipato kupitia kilimo cha mbogamboga hata kama una mtaji mdogo.Anza na sehemu ndogo tu unayoweza kupata hata kama ni nyumbani.

### 5. UFUGAJI WA NDEGE (KUKU, BATA, N.K)

Hii ni biashara ambayo ina faida kubwa lakini pia ina changamoto zake kama vile kuku wako kufa.
Vifo vya mifugo huwaumiza sana wafugaji na mara nyingi husababishwa na mifugo hiyo kula uchafu.
Hivyo, unapoingia kwenye ufugaji jitahidi uwe na mazingira safi na salama kwa mifugo yako.
Usafi wa mara kwa mara hasa hasa kwenye malisho yao utahitajika.
Kwa vile mtaji ni mdogo, unaweza kuanza na kuku wa kienyeji, bata. Japo kuwa wanachukuwa muda ila kuwa mvumilivu, faida utaiona.

### 6. UREMBO (MAKEUP, KUSUKA & KUCHA)
Urembo ni gharama. Wanadada wanataka kupendeza wanapokwenda safari zao kama ni kazini ama shughulini.
Uzuri ni kwamba hii ni biashara ya kila siku unayoweza kufanya, kufanya makeup, kutengeneza kucha na ususi wa nywele zinalipa vizuri tu.
Kuna watu wengi tu wanaendesha maisha yao kupitia biashara hizo. Kwanini wewe ushindwe? Na kama sio mtaalamu, hakuna tatizo, chukua muda wako na kujifunza, ndani ya muda utaweza.

### 7. KUPANGA SHEREHE/MATUKIO (EVENT PLANNING)
Kuanzia maharusi, kitchen party, sandoff na sherehe nyenginezo nisizozifahamu. Zote hizi ni fursa ambapo unaenda kusaidia watu kuandaa sherehe zao mwanzo mpaka mwisho.
Wewe ndio unaumiza kichwa kutafuta watu na huduma mbalimbali kama vile wapambaji, ma dj, au kuwatafutia gari ya kukodi, kuwapikishia chakula na megine mengi.
Unachohitaji kuweza kufanya biashara hii ni uwe unawajua watu husika wanaotakiwa kwenye sherehe hizo.
Mfano, ujue wapambaji wa ukumbi, wapishi wa maharusi, ma dj ili uweze kuwapa kazi hizo. Utalipwa kwa kufanya kazi hiyo.

### 8. USHONAJI NGUO
Kama wewe ni mpenzi wa mitindo, unaweza tengeneza kipato kizuri kwa kuwashonea watu nguo.
Itakuchukuwa muda kujifunza kushona ila ni kazi moja nzuri. Unapata kuwa mbunifu katika kutengeneza mishono mbali mbali na mwisho wake kulipwa.
Kama huna cherehani nyumbani, unaweza kwenda kukodi na kufanyia kazi zako hadi utakapo nunua yako.

### 9. KUFUNDISHA
Unaweza kufundisha chochote kila unachokijua ikiwa kuna watu wanataka kujifunza.
Jitathmini kwa kujiuliza, je ni kitu gani nakijua ambacho watu wanataka kujifunza? Hiyo ni rasilimali tosha.
Watafute hao watu na uwape huduma zako. Taaluma sio lazima iwe kufundisha hisabati na kemia tu, kama unajua kupika vizuri, kushona au chochote kile basi wafundishe watu.

### 10. KUTENGENEZA SIMU/KOMPYUTA
Watumiaji wa vifaa kama vile simu na kompyuta huzidi kila siku.
Vifaa hivi vinapopata tatizo kama vile kuingia loki sio kila mtu anaweza kutengeneza mwenyewe.
Hiyo hukupa wewe fursa ya kuwatatulia matatizo yao kwa kiasi cha pesa kadhaa. Unaweza kujifunza jinsi ya kutengeneza matatizo sugu ya simu kwenye mtandao. Kama kuna mtu karibu akufundishe na ujitangaze watu wa karibu wajue kuwa unafahamu ujuzi huo wa kurekebisha simu, wanawake wengi sasa ni mafunzi wa simu na kompyuta

### 11. UNYOZI WA NYWELE kwa WANAWAKE NA WATOTO TU
Hii pia ni biashara isiyokuwa na msimu kwavile nywele huota kila siku.
Jifunze kunyoa watu nywele halafu anza na wale wakaribu yako kama vile marafiki na ndugu. Unaweza pia kuajili kijana akanyoa hata wanaume ikawa inasaidia kuongeza kipato na huduma kwa wengi.
Utakapofanya kazi nzuri hao watakuwa wateja wako wakujirudia na pia kukutangazia huduma zako kwa watu wengine.

Unachohitaji ni kununua mashine ya kunyolea ambayo unaweza kupata kwa chini ya elfu hamsini.

### 12. KUUZA VOCHA ZA SIMU

Vocha! Tunanunua karibia kila siku.
Faida yake sio kubwa kihivyo ila ukizingatia kazi ni ndogo ya kufanya kwasababu vocha zinajiuza zenyewe.Vocha sio kitu cha kutumia nguvu kuuza muhimu watu wajue tu kama unauza vocha.
Unaweza kuona vocha zinauzwa kila sehemu kwamba utakosa wateja … lakini sio kweli, kuna sehemu nyingi tu ambazo hakuna muuza vocha karibu.Anza kuwauzia watu unaoishi nao, majirani au hata wanafunzi wa chuo.

### 13. UFUGAJI WA SAMAKI

Ufugaji wa samaki uko wa aina mbili, kuna samaki wa kula na wale wa mapambo. Hapa nitaongelea samaki wa mapambo kwa vile wana gharama ndogo na pia faida kubwa. Unaweza anza na samaki wawili au wanne na kuwatunza. Wakizaliana na kuwa wengi, uza baadhi yao.

### 14. KUKUZA MITI YA MAUA

Maua hupendezesha nyumba na wengi huamua kupanda nyumbani kwao.
Fuatilia jinsi gani maua tofauti yanavyopandwa na kisha yapande.
Kwa wastani, mti mmoja wa maua huuzwa kuanzia elfu mbili. Mtaji mkubwa hapa ni muda wa kupanda na kuishughulikia hiyo miti.

### 15. KUFANYA USAFI MAJUMBANI NA MAOFISINI

Watu wengi wamebanwa na kazi, na muda wasiokuwa kazini wana mambo mengi ya kufanya.
Unaweza kuwafanyia usafi na wakakulipa. Ni vizuri ukanunua vifaa vyako ambavyo sio ghali ila sehemu nyingi watakuruhusu kutumia vifaa vyao vya usafi.
Biashara ikiwa kubwa, unaweza amua kutafuta vifaa tofauti tofauti vya kufanyia kazi kitaalamu zaidi na kuajiri wasaidizi

### 16. KOCHA WA MAZOEZI KWA WANAWAKE WENZAKO

Nathubutu kusema kuwa hakuna kitu chenye thamani kwenye maisha kama afya nzuri. Watu wengi wanashtuka sikuhizi juu ya umuhimu wa kula vizuri na kufanya mazoezi. Hivyo, baada ya kupata elimu nzuri ya mazoezi, anza kuwafundisha watu. Utalipwa kwa ujuzi na muda wako.

### 17. KUPAMBA MAHARUSI

Hivi, nani hapendi kupendeza siku ya harusi yake? Hamna. Na ili kupendeza harusini, wanandoa inabidi wapambwe. Tafuta mtu anayepamba maharusi na muombe kumfanyia kazi (ikiwezekana bila hata malipo). Baada ya muda utajifunza vitu vingi vitakavyo kusaidia kuwa mtaalamu wa kupamba maharusi.

### 18. KUWAUZIA WATU BIDHAA ZAO

Kwa akili ya kawaida, ni rahisi mtu kukulipa unapomtengenezea pesa.
Jifunze kuuza kisha tafuta watu wenye biashara na uwaambie kuwa unaweza kuwaletea wateja kwa malipo mutakayokubaliana.
Hii ni biashara nzuri kwasababu unatengeneza kipato kwa kutumia fedha ya mtu mwengine. Unachohitaji ni ujuzi wa kuuza vitu.

### 19. KUTENGENEZA SABUNI ZA MAJI

**Unaweza kutengeneza sabuni za maji kama:**

1. Sabuni za kunawia mikono
2. Sabuni za usafi wa chooni
3. Sabuni za kufulia.

Ukitaka kuanza utengenezaji kuwa makini kwa kuvaa gloves na miwani kuzuia kemikali zisikuathiri mikono na macho.

## JINSI YA KUTENGENEZA SABUNI ZA KUNAWIA MIKONO

MALIGHAFI

1. Sulphonic asid - Inafanana na asali
2. Siless - Kuimarisha povu la sabuni,sabuni iwe imara
3. Soda ash - Inang'arisha sabuni,kuongeza povu
4. Formalinge - kuuwa bacteria, sabuni kukaa kwa muda mrefu.
5. Rangi - Kuongeza uzito wa sabuni
6. Maji -Kibebeo inabeba sabuni yote
7. Griseline - Inarainisha ngozi, mikono
8. Perfume -Inaleta harufu nzuri ya sabuni/
9. Chumvi

## HATUA ZA KUTENGENEZA

1. Maji lita 10 yaliyochujwa
2. Sulphonic acid vijiko 3 vya chakula
3. Koroga kwa dakika 5-15 kulia au kushoto
4. Siless ½ lita weka kwenye chombo husika changanya koroga
5. Formalinge kijiko 1 cha chakula koroga
6. Griseline vijiko 3 vya chakula koroga
7. Rangi ½ kijiko cha chai koroga /kijani/Bluu
8. Soda ash vijiko 2 vya chai weka katika sabuni koroga
9. Chumvi Robo 3 koroga pembeni mimina, endelea kukoroga chumvi inaleta uzito kwenye sabuni endapo itakuwa nzito zaidi ongeza maji koroga.
10. Perfume weka vijiko 2 vya chakula koroga tayari kwa matumizi iache ipoe kwa masaa 2 na fungasha kwenye vifungashio.

**NB**. Funika sabuni kuzuia harufu perfume kupotea.

## KUTENGENEZA SABUNI YA CHOONI

**MALIGHAFI**

1. Maji lita 10.
2. Sulphonic asid ½
3. Siless vijiko 5 vya chakula
4. Formalinge vijiko 5
5. Chumvi ¼ ilo, kuongeza uzito
6. Sodaash vijiko 4 vya chakula
7. Rangi kijiko 1 cha chakula
8. Perfume vijiko 2 vya chakula

## JINSI YA KUTENGENEZA/ HATUA ZA KUTENGENEZA

1. Weka maji lita 10.

2. Sulphonic acid 1/2 lita.
3. Siless - vijiko 5 vya chakula
4. Formaline vijiko 5 vya chakula
5. Rangi kijiko 1 cha chakula
6. Chumvi 1/4 kilo
7. Sodaash vijiko 4 vya chakula
8. Perfume vijiko 2 vya chakula

Koroga dakika 20-30 na uhakikishe hakuna weupe wa mabonge ndani ya dawa yako.

**NB:** Funika acha kwa masaa 2 ipoe weka kwenye vifungashio.

## UTENGENEZAJI SABUNI ZA MCHE

***(sabuni za magadi au Gwanji)***

1. Kuna sabuni ambazo zina harufu (perfumE) na ambazo hazina.

-Povu jingi la kutosha
-Iwe haina mwasho
-Rangi (bluu)
-Iwe ngumu
-Iwe imara
-Iwe na shepu nzuri inayoweza kuvutia mteja.

**MALIGHAFI**

1. Cost soda(itunzwe juu ya kitu kama mbao ukiweka chini inaganda
2. Mafuta, Mbosa,(Mise), mawese,kolie,alizeti.
3. Hydrogen peloc side - kugeuza mafuta, sabuni kuwa nyeupe ing'ae kuipa imara
4. Sodiam silicate- kuondoa muwasho.
5. Hydrometer- kifaa kinachotumika kupima kiwango cha joto kinatakiwa kiwe kuanzia nyuzi joto 28 hadi 30
6. Meza hutumika kukatia sabuni
7. Box, umbo la sabuni , box la mbao hutengenezwa kwa kufuata vipimo vya sabuni ni urefu, upana na kina .
8. Kisu ,kamba, karatasi la nailoni kuzuia uji wa sabuni usivuje endapo box lina matundu.

## JINSI YA UTENGENEZAJI SABUNI ZA GWANJI/MCHE

**MALIGHAFI**

1. Mafuta lita 20
2. Maji yaliyochanganywa na costic soda lita 10
3. Bluu vijiko 6 vya chakula
4. Vaa glovus
5. Maxic/puani
6. Gamu boot.

**JINSI YA KUCHANGANYA COSTIC NA MAJI**

-Pima maji lita 10
-Cost soda lita 4kg
-Koroga maji na costic mpaka iyeyuke costic,
-koroga kwa muda wa dakika 40-45 kwa kutumia mwiko mrefu.

- **ANGALIZO**

-Hakikisha umevaa vifaa tajwa hapo juu.
-Hakikisha unakorogea mahali palipo na hewa ya kutosha costic ni hatari sana, hakikisha isikirukie wakati wa kukoroga pia hakikisha usishike kwa mikono mitupu kama imetokea imekudondokea bahati mbaya osha kwa maji haraka sana.

**HUDUMA YA KWANZA**

-Maji
-Baada ya kukoroga kwa dakika 40 - 45 utaiacha kwa muda wa masaa 24

- **ANGALIZO**

-Weka sehemu isiyoingiwa na watu mara kwa mara ni hatari.
-Baada ya kupoa unachukua kipimo ambacho ni Hydrometer temperature ni kipimo kinchopima joto hakikisha Hydrometer imesoma nyuzi joto 280,29 -30.

**JINSI YA KUFANYA**

- Andaa box la mbao
- Karatasi ya mpira ya bluu - mita 2 ½
- Ndoo kubwa 2 na dyaba.

1. Chukuwa mafuta lita 20 unamimina kwenye ndoo kubwa, mafuta yaliyoyeyuka sio mgando.
2. Chukua maji yaliyochanganywa na costic soda yenye nyuzi joto 30? unamimina kwenye ndoo yenye mafuta , unamimina kidogo kidogo huku mtu mwingine akiendelea kukoroga kwa kutumia mwiko mrefu, koroga kwa dakika 30 huku ukiwa unaandaa box umeliwekea karatasi ndani ya prastic /mpira. Baada ya dakika 30 kuisha utamimina uji uliokoroga kwenye box hilo. Baada ya kumimina utaweka rangi.

**MFANO WA BOX LA KUTENGENEZEA SABUNI YA MCHE**



**JINSI YA KUWEKA RANGI.**

- Rangi ya bluu
- Rangi ya mafuta

1. Chukua mafuta kidogo robo lita
2. Pima vijiko 6 vya chakula vya rangi ya bluu
3. Changanya na mafuta robo lita koroga mpaka ilainike pembeni.
4. Changanya, mimina kwenye box lenye uji huku ukiwa na kibao kirefu kama fimbo una kata mistari ili kuweka mawingu.

MCHANGANYIKO UNAMIMINWA KWENYE BOX(MOULD) ILI SABUNI IPATIKANE



5. Acha ipoe kwa muda wa masaa 24 . Baada ya masaa 24 sabuni iko tayari kwa matumizi!.

Ondoa ndani ya box baada ya kukauka vizuri na kuwa ngumu kisha kata miche kwa saizi unayotaka.





## BIASHARA YA VIUNGO KWA AJILI YA VINYWAJI NA CHAKULA

Viungo(Spices) ni kama zifuatazo:-

(Mdalasini) Cinnamon



(Uzile) Cumin



(Tangawizi) Ginger



(Pilipili Manga) Black pepper



(Hiliki) Cardamon



(Mchaichai) Lemons Grass



(Karafuu) Cloves



(Vanila) Vanilla



(Kungu Manga) Nutmeg



(Bizari) Turmeric



(Giligilani) Coriander



(uwatu) Fenugreek



(zahatari) Thyme



## SPICES NI TIBA

Familia ikila na kuzingatia kanuni za lishe itakuwa imara na mwili kuwa na kinga kiasi kwamba maradhi nyemelezi yataepukika kwani kinga ni zaidi ya tiba. Lishe uzingatia afya ya mlaji na kuhakikisha kila kinywaji kina faida mwilini pamoja na kushiba. Spices nyingi zina sifa ya tiba. Kwa hiyo biashara yake ina faida kwako na jamii.

**(Masala):- Spices Combination**
Tea Masala
Fish/Meat Masala

Spices Gift Packs
-Oils Extracts
-Herbal Soaps

## VIFUNGASHA NA KUWEKA LEBEL




Spices zinatunzwa kwenye vifungasha mbali mbali ili kuvutia wateja. Vifungasha vina aina mbali mbali kuanzia mifuko, chupa za plastic, glasi. Kisha weka lebo nzuri ya rangi kuogeza mvuto kabla ya kuingia sokoni



 


## FAIDA YA KUFUNGASHA NA KUWEKA LEBO NZURI KWENYE SPICES

- Kutunza vizuri ziwe salama na zikae kwa muda mrefu bila kuharibika
- Kuvutia wateja kwa muonekano ili wakishatumia waonje na kuhisi ubora
- Kuzuia wadudu waharibifu ili wasiharibu spices na kuondoa ubora wake

## UTUNZAJI WA SPICES ZILIZOTAYARI

Hakikisha unapaki kwenye kifungasha zikiwa mpya na zimekauka vizuri bila unyevu unyevu
Hakikisha hakuna vumbi na zinapotunzwa pawe pakavu na salama
Hakikisha vifungasha na mifuniko yake iko imara na haijapasuka au kama ni kufungwa vimefungwa na kubana vizuri
Hakikisha unatumia vifungasha vyenye uajzo tofauti ili kukidhi mahitaji ya wateja kuanzia kiwango cha chini hadi cha juu
(Mfano. Funga gram 100, Nusu Kg, Kg na hata vidogo vidogo vya gram 50 kwa watu wenye uwezo mdogo wa kipato)

## UTAFUTAJI WA MASOKO

### Soko ni nini?

Soko ni utaratibu au mtindo uliowekwa kwa mujibu wa kanuni /sheria kumwezesha mfanya biashara kuuza bidhaa zake kwa wateja/walaji. Husaidia kupanga nini uuze,nani umuuzie au jinsi gani watu wanavyoweza kujua kitu gani unauza,hivyo kukuwezesha kuzalisha kile ambacho kinahitajika katika soko sahihi.

Mafanikio katika biashara hutokana na mwonekano wa kipekee wa bidhaa au bidhaa unayozalisha kukidhi matakwa ya walaji au wateja pia kuweza kutambua aina fulani ya watu ambao wangependa kununua bidhaa yako na kuweza kueleza bayana ni kitu gani, watu wategemee kunufaika kwa kunua bidhaa zako kati ya kundi hili la walengwa.

Kwa kifupi soko ni MTEJA wa bidhaa na huduma uayozalisha

**Soko lako ni;**

- Wateja wako ulionao kwasasa
- Wateja unaotarajia kuwapata baadae
- Wateja uliopoteza na untarajia watakurudia tena

**Masoko ni nini?**

Masoko ni shughuli yoyote ile anayofanya mfanyabiashara ili kuimarisha biashara yake.

Haitoshelezi tu kukaa kungojea oda.

Mfano wa shughuli hizo ni;

- Kuelewa matakwa ya wateja wa bidhaa yako
- Kupanga bei ambayo wateja watakuwa tayari kulipa na itakupa faida
- Usambazaji wa bidhaa au huduma kwa wateja wako
- Kuwavutia wateja wanaume bidhaa au huduma yako

**5.2. UTAFITI WA SOKO**

1. **1. Kwa nini tujifunze kuhusu soko?**

a) **Mahitaji (demand)**

Waswahili husema '**unaweza kumlazimisha punda aende mtoni lakini huwezi kumlazimisha anywe maji'**ina maana bidhaa zako kuwa wakati soko halihitaji bidhaa zako huwezi kulazimisha bidhaa yako inunuliwe

b) **Bidhaa sahihi –** usijaribu kumuuzia kitana mtu mwenye kipara bali muuzie kofia

c) **Kufuata mkumbo**-ni vema kutofautisha bidhaa za kuuza kwa wateja

**2. Unahitaji kufahamu nini kutokana na soko lako?**

Maswali yafuatayo ndio yakusaidia kufanya utafiti wa soko lako

- Wateja wako ni akina nani?
- Wako wapi
- Mahitaji yao ni nini?
- Wanapendelea nini kutokana na bidhaa zako
- Ni mara ngapi na kiasi gani a wanacho nunua?
- Wana nunua wakati gani?
- Ni kiasi gani cha pesa wako tayari kutoa?
- Ni jinsi gani bidhaa zitawafikia wateja
- Washindani wako ni wapi?
- Ubora wa bidhaa zao na bei zao vikoje

**NB; kutafuta majibu ya maswali haya kunaitwa utafiti wa masoko**

**3. Jinsi ya kufanya utafiti a soko**

Mbinu zifuatazo zinaeza kutumika kufanya utafiti wa soko la bidhaa au huduma unazozalisha:-

- Kupitia Kwa wateja (kusikiliza maoni yao, kuachunguza na kuwauliza maswali).
- Kuwauliza maswali watumiaji mbali mbali wa bidhaa zako ( nini wanachohitaji na wasicho kihitaji, mapendekezo na nini kiongezwe)
- Kwa marafiki na ndugu
- Kusoma kwenye vitabu, magazeti, kusikiliza radio na kuangalia televisheni
- Kupeleka bidhaa zako katika maonesho ya biashara
- Kuangalia biashara za washindani wako: bei, ubora, tofauti za bidhaa,, kuonesha bidhaa, na huduma zinazoambatana na bidhaa zako

- Onesha sampuli ya bidhaaa au tembeza sampuli ya bidhaa na waulize watu maoni juu ya bidhaa zako

**4. Jumuisho la masuala ya masoko**

**B-Nne katika masoko**

- Bidhaa
- Bei
- Banda
- Bango

a) **<u>BIDHAA</u>**- Bidhaa ni kitu chochote kinachozalishwa kwa ajili ya kuuza au kutumia.

**<u>Sifa za bidhaa</u>**

Bidhaa nzuri ni ile inayoridhisha na inakidhi matakwa ya soko. Kwa mfano:-

- Ubora(muda, malighafi nzuri, iliyotengenezwa vizuri)
- Yenye kuvutia ( rangi,mapambo,usafi, utengenezaji mzuri)
- Mtindo (umbile zuri, inahusiana na thamani,saizi)
- Ya kisasa (Inayoendana matumizi ya mtindo uliopo- fassion)
- Tofauti na bidhaa za ashindani

**b) <u>BEI</u>**- Bei nithamani ya bidhaa au huduma ambayo mteja yuko tayari kumudu au kulipia. Kwa hiyo bei hujumuisha Gharama zote na faida au Bei huiumuisha gharama za ununuzi, gharama za uendeshaji na faida.

**<u>Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kupanga bei</u>**.

- Ghrama zote kwa jumla (gharama halisi)
- Bei za wapinzani
- Mahali ulipo kiasi ambacho wateja wako radhi kulipia kwa kutegemea uwezo wao kifedha)
- Msimu (kwa mfano bei kubwa za vinyago msimu wa watalii au bei ndogo za fenicha wakati wa mvua )
- Kupata faida ya kutosha kuendesha shughuli bila matatizo

**c) <u>Banda au mahali pa kufanyia biashara</u>**

Banda ni mahali muhimu sana katika kuuza bidhaa au huduma. Mahali pa kufanyia biashara panatakiwa pawe na sifa zifuatazo:-

- Rahisi kufikiwa na wateja
- Usalama, usafi
- Sehemu ya maegesho
- Kuwa karibu na huduma nyingine muhimu kama vile usafiri wa daladala, sehemu za vinywaji, vyakula,umeme n.k
- Yenye mwanga wa kutosha
- Rahisi kuonekana
- Huduma hutolewa saa zote

**5. Upangaji mzuri wa bidhaa mahali pa biashara.**

- Bidhaa zipangwe kwa seti
- Mahali pa wazi panapoonekana kiurahisi
- Weka bidhaa chache katika makundi madogo madogo
- Weka bidhaa za aina mbalimbali
- Panga sehemu yenye mwanga wa kutosha
- Sehemu safi
- Tumia picha au katalogi

**6. BANGO AU UVUMISHAJI**

Uvumishaji unajumuisha shughuli kadhaa ikiwa ni pamoja na uvumishaji wa mauzo,utangazaji,uhusiano wa jumuia na mbinu za kuuza. Shughuli hizo zinasaidia kuwavitia wateja, lakini hasahasa zinawapa wateja imani na bidhaa zako kuhakikisha kuwa hawanunui kwa mtu mwingine.Jambo muhimu la kuzingatia katika uvumishaji wa bidhaa ni lazima uwe mchangamfu na kuwa macho kuvutia wateja.

**Kuvumisha mauzo(sales promotion)**

- Punguza bei yako kidogo ili wateja waone kuwa ni ndogo. Mfano:- shs 999.00 badala ya 1000.00
- Weka bei maalum wakati wa sikukuu mbalimbali
- Panga bidhaa madirishani ilizionekane kwa nje (display)
- Uza bidhaa zinazoendana. Mfano muuza maandazi anaweza kuuza chai au muuza sukari anaweza kuuza majani ya chai

**Utangazaji**

Radio, magazeti,tv,sinema,mabango,kadi za biashara za mwenye biashara(business card)na sifa zinazotolewa kwa njia ya mdomo na watu waliokwisha kutumia bidhaa hizo.

**Mahusiano**

Kuchangia huduma za jamii Kama vile elimu, afya mazingira n.k

**Mbinu za uuzaji**

- Jinsi ya kutambulisha bidhaa, eleza faida za bidhaa na ubora wake
- Kumthamini mteja
- Eleza faida ya bidhaa yako kabla hujataja bei
- Jaribu kuuliza juu ya mahitaji ya mteja ili uweze kumwelekeza kwenye bidhaa itakayomfaa.
- Kama mteja akiuliza bidhaa ambayo huuzi , unamwekeza zinapoatikana.

## KUTUMIA SIMU NA MITANDAO YA KIJAMII KUTANGAZA BIASHARA

Kutokana na matumizi ya TEHAMA katika mawasiliano, inabidi pia tutumie simu, computer na zana zote za mawasiliano kufikisha matangazo ya biashara yetu kwa watu kwa gharama nafuu sana.

Siku hizi simu janja(smart phone) wanazo watu wengi imekuwa rahisi kusambaza ujumbe, picha na video za sauti kupitia WhatsApp, Facebook, Instagram, Telegram, n.k kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

Bidhaa au huduma yaweza kusambazwa kwa mamilioni ya watu kwa gharama kidogo na ukapata oda za bidhaa zako kama zina uhitaji kwa watu popote duniani walioko kwenye mitandao ya kijamii .

Pia malipo yanalipwa kwa  mtandao mfano Mpesa, Airtel Money, Tigo pesa, Visa Card, n,k bila hata kumuona mteja aliyenunua bidhaa yako.

## LIPI LA KUFANYA KUTANGAZA BIASHARA MTANDAONI?

Kutengeneza akaunti ya Facebook, Instagram, n.k.kisha kupiga picha bidhaa na kuandaa tangazo lako ukiwambia wateja umuhimu wa bidhaa au huduma yako katika maisha yao na inabidi uelezee faida ya bidhaa yako(value) kwao endapo watanunua na kutumia.
Wateja hawanunui muonekano(features) bali wananunua thamani (value) ya bidhaa au huduma. Hakikisha unaweka namba yako ya simu n sehemu ya kukupata kwa wepesi. Toa maelezo kwa ufupi na maandishi makubwa yanayosomeka kwa wepesi.




Facebook na instagram kuna pia huduma ya kulipia tangazo na ukahamua liwafikie watu wengi wa eneo fulani, mfano. Ukiamua Tanga na Kilimamjaro na watu wa umri Fulani na idadi Fulani  wone tangazo lako la bidhaa au huduma yako.




Kwa hiyo tunaweza kutangaza biashara yetu kwenye mitandao ya kijamii tukiwa na akaunti zetu au za kampuni zetu. Kama huna akaunti facebook na Instagram ifunngue na kisha anza kutangaza biashara yako na huduma utowazo.

Fungua facebook na jaza yanayotakiwa kwa akaunti mpya kama unavyoona hapa chini




Kama kwenye simu yako haipo nenda playstore na pakua kisha install na hapo utafungua akaunti yako kwa hatua zote. Pata ujuzi kwa wazoefu namna ya kuitumia facebook na Instagram kutangaza biashara.

## BLOG NA TOVUTI(website) KATIKA KUTANGAZA BIASHARA




Kwanza elewa neno WWW ni nini:

WWW ni kifupisho cha neno zima WORLD WIDE WEB - si umeona websites nyingine zinaanza na www, basi www ni kifupisho cha World Wide Web. Kwa lugha rahisi WEB ni namna maalum ya ku share taarifa kupitia internet kwa kuunganisha mawasiliano toka kompyuta tofauti tofauti ulimwenguni.

Kwa mujibu wa Wikipedia, neno blog ni kifupisho cha neno Web LOG, yaani rekodi au usajili wa taarifa za mara kwa mara ndani ya WEB. Ili kufupisha neno zima WEB BLOG wakaita kwa kifupi BLOG.

Mfano wa website(tovuti) ni : [www.bakwataonlineacademy.ac.tz](http://www.bakwataonlineacademy.ac.tz) **hii tunaitumia kwa ajili ya mafunzo na kozi mbali mbali kutangazwa kwa watu wengi duniani kwa kupitia tovuti hiyo.**

Kwa hiyo unaweza ukajifunza kuandaa blog yako au kumpa mtu kazi akuandalie na utangaze biashara yako ili watu wakitafuta katika google kitu kinachohusiana na huduma zako blog yako iwe katika list na kukupata kwa haraka ili wapate huduma yako. Pia unaweza kuwa na website ya biashara yako kwa kutumia mtaalam wa kutengeneza website na ukamlipa kiasi cha fedha na kisha ukalipia jina na kuitunza kwenye seva ili watu wengi waione kwenye mtandao na kupata habari za biashara yako. Kampuni, asasi za kiraia, watu binafsi, vyuo, mashule na taasisi nyingi siku hizi zina website na blog ili kufikisha habari zake kwa watu wengu kwa wepesi zaidi.



## MTIHANI WA KWANZA 2021- MTIHANI WA WAZI

## Jibu maswali yote 10, Andika Jibu sahihi

1. Nini wajibu wa  mwanamke katika uislam

A. Kuzaa na kufanya kazi za nyumbani
B. Kulea watoto na kuwafundisha tabia nzuri
C. Kumcha Mungu, Kujiheshimu na Kusaidia katika familia kimalezi
D. hakuna jibu sahihi

2. Mwanaume anawajibu gani kwa mwanamke katika uislam?
   A. Kumtunza na kumhifadhi
   B. Kumtunza, kumuongoza, kumuheshi na kumhurumia kwa mapenzi ya dhati
   C. Kuhakikisha hatoki ndani na hafanyi kazi ambayo hataki
   D. Kuhakikisha anapika, anazaa, anafua nguo na akikosea ampige viboko na kumtenga kitandani

3. Chakula cha wanga na sukari kina faida gani mwilini?
   A. Kuongeza kinga na mafuta mwilini
   B. Kulinda mwili
   C. Kuongeza nishati na joto mwilini
   D. Hakuna jibu sahihi
4. Lipi kundi la  vyakula vyenye protein katika vyakula vifuatavyo
   A. Mchicha, Nyanya na Karoti
   B. Karanga, nyama na Maharagwe
   C. Parachichi na tango
   D. Andazi, Chapati na Ndizi
5. Mtu alikuja kwa Rasuli wa Allaah (Swalla Allaahu alayhi wa salam) na akasema:

"Ee Rasuli wa Allaah! Nani miongoni wa watu wote anastahiki uhusiano wangu wa karibu?" Nabiy akajibu.  "     "Chagua jibu sahihi

   A. Baba yako
   B. Mama yako
   C. Mjomba
   D. Rafiki
   E. Mke au Mume
6. "...Hakika sitapoteza amali ya mtendaji mema miongoni mwenu awe mwanamume au mwanamke." Sura ya ngapi na ni aya ya ngapi ndani ya Qur'an
   A. (3:195)
   B. (4:7)
   C. (7:8)
   D. (23:4)
7. Elimu ni wajibu kwa :
   A. Wanaume tu
   B. waislam wote wakiwemo wanawake na wanaume
   C. Walio soma dini tu
   D. Kwa anayetaka kusoma dini
8. Elezea unavyoweza kutangaza biashara  kwa watu wengi na ukatumia ghama kidogo

9. Tofautisha kati ya Bidhaa na huduma, Toa mifano ya bidha na mifano ya huduma

   Elezea maana ya chakula na lishe

**-MWISHO-**